# Nipashe

Jumamosi Februari 17, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581589

MWANGA WA

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**MBAPPE RASMI ANAONDOKA PSG**

UKURASA 21

**HUKUMU** mke wa Bilionea Msuya yapigwa kalenda

UKURASA 4

**MAHAKAMA** yaelezwa wakili feki alivyonaswa

UKURASA 5



**KIGEZO** vyeti JKT na JKU ajira vijana chaondolewa

UKURASA 5

# Mambo 13 alama kwa Lowassa kukumbukwa




**VILIO**, simanzi vyatawala kuagwa mwili Monduli...

*Endelea ukurasa 2 & 4*

## Bunge laitega serikali mgawo umeme

UKURASA 3



Maria Ngoda (katikati), aliyekuwa amehukumiwa jela miaka 22 na Mahakama ya Hakimu Mkazi Iringa kwa kukutwa na ndoo yenye vipande 12 vinavyosadikika kuwa nyama ya swala, akisindikizwa na askari Magereza baada ya kuachiwa huru katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Mjane vipande nyama ya swala aachiwa huru

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA, KMC FC VITANI MOROGORO** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Simanzi, vilio mwili ukiagwa Monduli

**Na Allan Isack**, MONDULI

MAELFU ya wananchi walijitokeza jana kuaga mwili wa Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Lowassa, nyumbani kwake kijijini Ngarash, Monduli mkoani Arusha.

Wakati wa tukio hilo, vilio na simanzi vilitawala kutoka kwa wanaume, wanawake na watoto walipopita mbele ya jeneza kutoa heshima zao za mwisho. Shughuli za kuaga mwili wa Lowassa nyumbani hapo ziliongozwa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda.

Akizungumza wakati wa ibada ya kutoa heshima za mwisho, Pinda aliwataka Watanzania kumkumbuka Lowassa kwa mambo mazuri aliyofanya katika nchi na taifa.

Alisema akiwa serikalini alifanya kazi vizuri na Lowassa na kuna mambo mengi aliyojifunza kutoka kwake.

"Hatua aliyofikia Edward Lowassa anahitaji kufanyiwa maombi ili Mwenyezi Mungu aweze kumfungulia milango ya mbinguni. Pia tujaribu kumkumbuka kwa mengi aliyofanya," alisema.

Pinda alisema Lowassa alikuwa anasimamia kile alichotaka kufanya katika utendaji kazi wake, hivyo alitoa rai kwa Watanzania kuiga mema aliyoyafanya na kuyaendeleza kama ishara ya kumkumbuka.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema Lowassa alikuwa mtu wa watu mwenye marafiki wengi na alifanya kazi iliyotukuka ndani ya serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM). "Kuna mambo aliyofanya ikiwemo kuacha alama kwa nchi yetu na Chama Cha Mapinduzi wakati akiwa mtendaji ndani ya serikali na chama," alisema.

"Sisi kama viongozi wa serikali tumebeba jukumu la kusimamia na kuhitimisha hadi hapo tutakapompumzisha na kumhifadhi kwenye nyumba yake ya milele," aliongeza.

Mhagama aliwaomba wananchi kujenga utamaduni wa kuwaombea viongozi katika utendaji kazi kwa kuwa wametwishwa jukumu la kuwahudumia.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara, Peter Toima, akitoa salamu za rambirambi kwa niaba ya wenyeviti wa CCM nchini, alisema Lowassa alikuwa mtu wa watu na kiongozi mahiri na makini.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Abel Mollel, alisema Lowassa alikuwa mshiriki mzuri na mwaminifu wa maendeleo ya kiroho kwenye madhehebu ya dini ya Kikristo na kwamba hata kwa dini nyingine alitoa michango yake.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), Balozi Ephraim Mafuru, alisema kituo hicho kinamkumbuka Lowassa kwa kuwa alipokuwa mkurugenzi mtendaji, alileta mabadiliko makubwa ikiwamo mageuzi katika sekta ya utalii na uchumi wa kumbi za mikutano ili kuwavutia wageni wanapoingia nchini kutembelea vivutio vya utalii.

Mkuu wa Mkoa wa Singida mstaafu, Parseko Kone, akizungumza kwa niaba ya marafiki wa familia ya Lowassa, alisema kiongozi huyo alikuwa mchapakazi na mwenye upendo.




Mfanyabiashara maarufu nchini, Rostam Azizi akitoa heshima za mwisho katika mwili wa Waziri Mkuu mstaafu Hayati Edward Lowassa katika kijiji cha Ngarash, Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mambo 13 alama Lowassa kukumbukwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

LINAPOTAJWA jina la Edward Ngoyai Lowassa, ni dhahiri pasipo na shaka kuna baadhi ya taswira ya mambo yanakuja ambayo kiongozi huyo aliyafanya na yatakuwa alama ya kudumu kwa kizazi cha sasa na vinavyofuata. Kwa maneno mengine, matendo yake yatabaki kuwa historia na alama ya kumbukumbu isiyofutika.

Mambo hayo ni yale aliyoyafanya kiongozi huyo ambaye Jumamosi iliyopita alihitimisha safari yake ya maisha baada ya kuaga dunia katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam.

Miongoni mwa mambo hayo, yalitajwa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akitoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge huku akibainisha kuwa Lowassa ataendelea kukumbukwa kwa rekodi kubwa ya kusimamia mambo yenye maslahi mapana kwa taifa.

**USAFIRI BODABODA**

Miongoni mwa mambo ambayo ni kikwazo katika kufanikisha shughuli mbalimbali ni usafiri hasa katika miji mikubwa ikiwamo Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma na Mbeya. Changamoto hiyo imewafanya watu wengi kushindwa kufika maeneo ya kazi na kurejea kwa wakati nyumbani baada ya kazi.

Kwa kutambua hilo, Majaliwa alisema Lowassa, enzi za uhai wake, ndiye aliyeruhusu biashara ya pikipiki kubeba abiria, hatua ambayo ilisaidia vijana wengi nchini kupata ajira.

**VYUO VYA UALIMU**

Majaliwa alisema mchango wa Lowassa aliyekuwa Waziri Mkuu katika Serikali ya Awamu ya Nne, ni pamoja na kusimamia uamuzi wa serikali kubadili vilivyokuwa vyuo vya ualimu vya Mkwawa na Chang'ombe kuwa vyuo vikuu vishiriki vya elimu.

**ZAHANATI, VITUO VYA AFYA**

Jambo lingine kwa mujibu wa Majaliwa, ni ujenzi wa zahanati na vituo vya afya katika ngazi za vijiji na kata.

Lowasa alihimiza ujenzi wa vituo hivyo vya kutolea huduma za afya akiwa Waziri Mkuu kutokana na serikali kuanzisha Mpango wa maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

**USIMAMIZI MMES**

Baada ya mafanikio makubwa katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), serikali ya awamu ya nne ilianzisha mpango kama huo kwa elimu ya sekondari (MMES). Katika mpango huo, ilisisitizwa kuwe na angalau shule ya sekondari katika kila kata.

Lowassa akiwa Waziri Mkuu, alisimamia ujenzi wa shule hizo, maarufu kama sekondari za kata na ndani ya uongozi wake akiwa Waziri Mkuu, ilishuhudiwa kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa vilivyochochea vijana wengi wa kitanzania waliomaliza elimu ya msingi kujiunga na sekondari.

**WAFUGAJI KUSOMA**

Jamii ya wafugaji wa kabila la Wamasai kwa miaka mingi imekuwa nyuma katika suala la elimu kutokana na utamaduni wa kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta malisho ya mifugo.

Kutokana na hali hiyo, Lowassa alikuwa mstari wa mbele kuhamasisha jamii ya wafugaji kupenda elimu kwa kuanzisha shule nyingi za sekondari katika maeneo yao, kutilia mkazo suala la elimu na kupiga vita mimba kwa wanafunzi pamoja na kuolewa wangali wadogo.

**UTATUZI KERO BALOZI**

Kwa mujibu wa Majaliwa, Lowassa akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, alifanikiwa kutatua changamoto za baadhi ya ofisi za balozi za Tanzania kuchelewa kupata mawasiliano, hususan pale balozi anapohitimisha muda wake.

"Alihakikisha kunakuwapo mawasiliano ya haraka pamoja na kutatua suala la 'diplomatic bags' kutoa majibu kwa haraka. Vilevile, Kamati hiyo ilianzisha utaratibu wa kutembelea ofisi za balozi zetu katika nchi mbalimbali, jambo ambalo lilisaidia kubaini changamoto na kuzitafutia ufumbuzi," alisema Majaliwa.

Hata hivyo, Nipashe katika uchambuzi wake limebaini kuna baadhi ya mambo ambayo Lowassa aliyafanya ama kushiriki ambayo yameacha alama hadi sasa

**MAJI ZIWA VICTORIA**

Suala la matumizi ya maji ya Ziwa Victoria yamekuwa ya vuta nikuvute kwa miaka mingi. Akiwa Waziri wa Maji katika Serikali ya Awamu ya Tatu, Lowassa alianzisha hoja na kufanikiwa kulishawishi Baraza la Mawaziri kukubali mpango wa kutoa maji katika Ziwa Victoria na kuyapeleka kwa wananchi wa mikoa ya Mwanza na Shinyanga.

Kabla ya kufanikisha azma hiyo, alikutana na ugumu kwenye mradi huo kutokana na mkataba wa zamani wa kimataifa kuipa Misri haki ya kumiliki Ziwa Victoria kwa sababu ya Mto Nile kuwa tegemeo la nchi hiyo.

**WALIMU 'VODA FASTA'**

Kutokana na kasi ya ujenzi wa shule za sekondari za kata na ongezeko la wanafunzi, kuliibuka upungufu wa walimu katika shule hizo. Hatua hiyo ilimfanya Lowassa akiwa Waziri Mkuu kuibuka na Mpango Maalum wa Kuendeleza Walimu (Crash Program) ili kukabiliana nao ambao ulibatizwa kama 'Voda Fasta'.

**UTATUZI MIGOGORO YA ARDHI**

Akiwa Waziri wa Ardhi, Lowassa alitatua migogoro sugu ya ardhi ya wawekezaji na wananchi waliokuwa wakigombea mashamba makubwa ya Valeska, mashamba ya maua ya Kiliflora lililoko USA-River, Kiliflora Nduruma na Blooms Chekereni.

**UTHUBUTU**

Wahenga wanasema ukitaka kufanikiwa ni sharti kuwa na uthubutu. Lowassa alikuwa mtu wa kuthubutu kutenda kila alichoamini kinawezekana na ndiyo maana watu wengi wamemwelezea kuwa hakuwa mtu wa kusitasita katika yale aliyokuwa anayapanga. Alikuwa akitekeleza.

**UFUATILIAJI**

Licha ya uthubutu, Lowassa alikuwa mtu wa kufuatilia mambo katika sekta alizokuwa akiziongoza ikiwamo alipokuwa Waziri Mkuu. Hatua hiyo ya ufuatiliaji ilimfanya awe mtu wa kutumia maneno 'naagiza', nataka', na 'naelekeza' badala ya neno 'naomba'.

**KUCHUKIA UMASKINI**

Lowassa katika maisha yake alikuwa mtu wa kuchukia umaskini kwa vitendo. Kutokana na dhamira hiyo, alikuwa mchapakazi akiamini kuwa kazi ndiyo msingi wa kufanikiwa katika kila jambo.

**KUJALI WANANCHI**

Maendeleo ndani ya Monduli yana mkono wa Lowassa hali inayodhihirisha kuwa alikuwa akijali wananchi na kushiriki kutatua shida na matatizo yaliyokuwa yakiwakabili.

## HABARI KITAIFA

# Mjane vipande nyama swala aachiwa huru

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Iringa, imemwachia huru Maria Ngoda, mkazi wa Isakalilo wilayani Iringa, aliyehukumiwa kifungo cha miaka 22 jela kwa hatia ya kukutwa na vipande 22 vya nyama ya swala.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Elvin Mgeta, baada ya kukubaliana na hoja zilizowasilishwa na mkata rufani na kutamka kuwa hana hatia na yuko huru.

Ngoda alipandishwa kizimbani jana majira ya saa 6:29 mchana kusomewa hukumu ya rufani yake iliyosajiliwa na Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS).

Awali, Ngoda alihukumiwa kifungo cha miaka 22 Novemba 3, 2023 na Hakimu Mkuu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Said Mkasiwa, baada ya kumtia hatiani.

Kutolewa kwa hukumu hiyo kuliibua mjadala kutokana na kidhibiti kilichodaiwa kuwa alikutwa nacho na idadi ya miaka aliyohukumiwa, hivyo ilisababisha makundi mbalimbali kupaza sauti, huku baadhi wakitangaza kumpa msaada wa kisheria kukata rufani.

Baada ya kutolewa kwa hukumu iliyomweka huru, Ngoda alisema: "Asante Mungu, nawashukuru ndugu zangu kunipigania. Mimi ni mama mjane na wanangu kwa kipindi hiki chote sijui walikuwa katika hali gani. Asante Mungu."

Pia alionekana akibubujikwa na machozi muda wote huku akiwashukuru wote waliomsaidia katika rufani yake. Akisoma hukumu kwa dakika 42, Jaji Mgeta alikubaliana na hoja 13 za wakata rufani ikiwemo ya ushahidi wa upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kosa pasipo kuacha shaka yoyote.

Jaji Mgeta alisema hoja zilizo wasilishwa na upande wa warufani zina mashiko ikiwamo suala la Ngoda kukosa uwakilishi wa kisheria wakati kesi yake ya awali inaendeshwa, huku upande wa mashtaka ukiwa na mawakili sita.

Hoja nyingine ni uthibitisho kama vipande vya nyama alivyokutwa navyo ni vya nyama pori, kwa maana ya swala kama ilivyodaiwa au la.

# Bunge laitega serikali mgawo umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeipa serikali miezi minne kumaliza tatizo la umeme hadi Juni, mwaka huu, kama ilivyoeleza awali licha ya kubadili ratiba yake kuwa mgawo utamalizika mwezi ujao.

Wakati bunge likitoa muda huo, serikali imesema tayari imekamilisha majaribio ya mtambo namba tisa katika Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 235 na mtambo namba nane wenye megawati zingine 235 unatarajiwa kuwashwa Machi, mwaka huu.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema jana bungeni kuwa: "Ratiba ya awali serikali mlisema Juni lakini mmerudisha hadi Machi, hivyo tunawapongeza. Bunge linawapa muda hadi Juni 2024, hivyo bunge litakapokuwa hapa mgawo uwe umeisha.

"Mmerudisha ratiba yenu nyuma na tunawashukuru sana kuliko watu waambiwe Machi halafu kukawa na siku mbili tatu za kusogea mbele basi tusogeze hadi Juni ili mambo yawe vizuri. Tunawashukuru sana kwa kazi nzuri," alisema.



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga,

Agizo hilo la Spika limetolewa baada ya Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Lupembe (CCM), Edwin Swale, ambaye alisema wabunge wanafahamu kuna miradi mingi ya kimkakati nchini ukiwamo Bwawa la Mwalimu Nyerere.

"Serikali ya awamu ya sita imefanya jitihada za kuhakikisha mradi huu unakamilika. Kumekuwa na taarifa mtandaoni kuwa pengine serikali leo ingezindua mashine mbili za mradi huu wa Mwalimu Nyerere. Je, nini kauli ya serikali juu ya mradi huu?" alihoji.

Naibu Waziri Kapinga, akijibu swali hilo, alisema mradi huo ni moja ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa kwa weledi mkubwa na Juni, mwaka huu, walitarajia kuwasha mtambo namba tisa kwa mara ya kwanza lakini kwa jitihada za serikali na ratiba yake ilirudishwa ya kuwasha mtambo huo mwezi huu (Februari).

"Naomba nilifahamishe bunge kwamba jana (juzi), tumefanikiwa kufanya majaribio kwa ukamilifu kwenye mtambo namba tisa ambao unazalisha megawati 235 na majaribio kama tulivyosema awali yatakamilika Februari 16 lakini kwa siku ya jana tumekamilisha kwa kiasi kikubwa sana.

"Kwa sasa wataalamu wetu wanaendelea na hatua za mwisho pamoja na kuweka ulinzi wa mtambo ili kuingia kwenye ratiba ya uzalishaji, lakini mwezi huu tuliahidi ratiba ya kuzindua mtambo huu na iko pale pale," alisema.

Kapinga aliliambia Bunge kuwa mtambo namba nane waliahidi kuuwasha Machi, mwaka huu, na ratiba itabaki kama ilivyo.

Hata hivyo, Spika Tulia alihoji mgawo wa umeme utaisha lini na Naibu Waziri Kapinga alisema matumizi ya umeme yanategemea matumizi ya kila siku.

"Tukizalisha mgawo wa umeme utakuwa umepungua kwa kiasi kikubwa lakini kwa kuwa mwezi huu Megawati 235 na mwezi ujao megawati 235 zitakuwa megawati 470, uhakika ni kwamba kufikia Machi, mgawo wote utakuwa umeisha," alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Chumbuni (CCM), Ussi Salum Pondeza, alihoji serikali ina mkakati gani wa kutangaza miradi mikubwa inayotekelezwa nchini ili wananchi, wakiwamo wa vijijini wafahamu.

Akijibu swali hilo kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema serikali inatumia njia mbalimbali zilizoainishwa katika Mkakati wa Mawasiliano wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) katika kutangaza utekelezaji wa miradi mikubwa inayotekelezwa nchini.

"Njia hizo ni pamoja na vyombo vya habari vya runinga kupitia vipindi maalum kama vile 'Tunatekeleza' (TBC) na 'Kurunzi ya Reli' (Reli onliveTV), redio na mitandao ya kijamii; maonesho ya biashara ya kimataifa ya sabasaba na maonesho ya kilimo nanenane.

"Aidha, niwaombe waheshimiwa wabunge kutumia mikutano yenu na wananchi majimboni kutoa elimu na uelewa kwa jitihada zinazofanywa na Serikali katika utekelezaji wa miradi hii mikubwa kwa kuwa ni jukumu letu sote," alisema.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD, IGALULA AUCTION MART AND COURT BROKERS, ASCERICS LTD,HOLLYNESS AUCTIONEERS, GADAU AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO.LTD,MCHINGA AUCTION MART ,JOMOK INVESTMENT CO.LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UBUNGO | MLIMO COMPANY LTD | NYUMBA | TIMOTH ANISETH KATWELA | KIMARA TEMBONI | 20/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | KIGODA ABBASI KIGODA | NYUMBA | KIGODA ABBASI KIGODA | VIGWAZA | 02/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | NWAKA BENI MWAKAPALILA | 1.NYUMBA 2.KIWANJA | NWAKA BENI MWAKAPALILA | 1. VETA -MBEYA 2. -ISYESYE-MBEYA | 06/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0754497397/0715868000**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.


## KUMBUKUMBU



**DIONISIA SIMON IVAMBI**

Dionisia umetimiza miaka 21 tangu ututoke ghafla tarehe 17/02/2003. katika maisha tulikupenda mno na katika kifo bado tunakupenda. mioyo yetu ilivunjika tulivyokupoteza na kutuachia majonzi yasiyofutika katika familia yetu. ingawa haupo nasi kimwili mdogo wetu lakini kiroho tuko pamoja nawe siku zote. bado tunakumbuka ucheshi, upendo na moyo wako wa kujitoa.

Dionisia unakumbukwa sana na wanao: nancy senior na diana dada zako veronica,, janeth, frida, kaka yako sebastian, shemeji zako, marafiki zako pamoja na wanafamilia wote.

Daima tunafarijika kwa maneno haya: sisi tulikupenda sana mdogo wetu lakini muumba wako alikupenda zaidi.

**Bwana alitoa na bwana ametwaa jina la bwana lihimidiwe**

HABARI KITAIFA

# Hukumu mke Bilionea Msuya yapigwa kalenda

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imesogeza mbele siku ya kutoa hukumu ya kesi ya mauaji inayomkabili mjane wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mwenzake Revocatus Muyella, maarufu kama Ray hadi Februari 23, mwaka huu saa 3:00 asubuhi.

Mjane huyo kwa mara ya kwanza alipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, Oktoba 23, 2016 akidaiwa kumuua wifi yake, Aneth Msuya, aliyeuawa Mei 26, 2016 kwa kuchinjwa nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam.

Aneth alikuwa mdogo wa Bilionea Msuya, aliyeuawa kwa kupigwa risasi eneo la Mijohoroni, Hai mkoani Kilimanjaro, Agosti 7, 2013.

Katika utetezi wake, Mrita alidai kuwa hawezi kumuua Aneth kwa sababu alikuwa kama mtoto wake wa kuzaa na kwamba alipoolewa yeye (Mrita) na mume wake walikabidhiwa wamlee tangu akiwa shule ya msingi Hukumu hiyo ilipangwa kutolewa jana na Jaji Edwin Kakolaki baada ya mahakama kumaliza kusikiliza ushahidi wa mashahidi 25 wa upande wa mashitaka, utetezi, vielelezo na kupitia vifungu vya sheria.

Desemba 11, 2023 wakati wazee wa baraza (Iddi Humba na Omary Panzi) wanatoa maoni yao, waliishauri mahakama iwaachie huru washtakiwa kwa sababu hawana hatia.

Mzee Humba alidai kuwa amepitia ushahidi wa mashahidi 25 na ushahidi wa upande wa utetezi katika mashahidi watano wa utetezi na kujiridhisha kwamba upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha shtaka bila kuacha shaka yoyote.

Mzee Panzi kwa upande wake, alidai kuwa baada ya kusikiliza pande zote anaunga mkono maoni ya mwenzake kuwa amejiridhisha kuwa upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashitaka bila shaka yoyote.

Jaji Kakolaki baada ya kusoma muhtasari wa ushahidi wa kila shahidi wa pande zote, alisema katika jinai kuna mambo makuu mawili ya kuangalia kitendo chenyewe ambacho mshtakiwa anakuwa anatuhumiwa kukitenda ni kwamba lazima kithibitike.

Pia alisema ni kusudio la mtu kutenda kitendo au kosa hilo na kwamba hayo mambo yote mawili ndiyo yanatengeneza kosa.

Katika maelezo ya onyo ya Miriam anadaiwa kueleza kuwa aliamua kumuua wifi yake kwa sababu alikuwa anamfuatafuata katika suala la usimamizi wa mirathi ya mumewe, marehemu Bilionea Msuya, na kwamba katika kutekeleza mauaji hayo, alimkodi mtu ambaye alimlipa Sh. milioni 20.

Maelezo hayo ya Miriam yalisomwa mahakamani hapo na shahidi wa kwanza wa upande wa mashtaka, Sajenti Mwajuma, aliyemhoji mshtakiwa huyo na kuandika maelezo yake alipotiwa mbaroni, baada ya kupokelewa mahakamani hapo kuwa kielelezo cha ushahidi wa upande wa mashtaka.

Hata hivyo, Miriam katika utetezi wake alikataa maelezo hayo na kudai kuwa kwanza hawezi kumuua wifi yake Aneth kwa sababu alikuwa mtoto wake wa kumlea tangu akiwa shule ya msingi hadi anaolewa na pia hakuwahi kuwa na ugomvi wa mali au mirathi na wifi yake huyo.

Shahidi wa 25 wa upande wa mashtaka, Getruda Mfuru, ambaye alikuwa dada wa kazi wa Aneth, alidai kuwa Mrita alimwahidi kumpa Sh. bilioni 50 kama angekamilisha kazi ambayo anaitaka kuifanya na dada yake.

# Serikali yabanwa ubovu wa barabara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameibana serikali kupeleka fedha za dharura kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara nchini kutokana na kuwa na hali mbaya inayosababisha wananchi kukosa mawasiliano na kushindwa kusafirisha mazao yao sokoni.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limeazimia serikali ikamilishe utoaji wa fedha za dharura kama ilivyoombwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ili kurekebisha miundombinu hiyo.

Hali hiyo ilijitokeza jana baada ya Mbunge wa Rorya (CCM), Jafari Chege, kumwomba Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kutoa hoja ya dharura kuhusu barabara zilizoharibika nchini zinazosimamiwa na taasisi hizo.

Katika hoja yake, Chege alisema barabara zinagusa uchumi wa kila mwananchi katika eneo husika na ni sehemu ya kujenga siasa na kwamba changamoto ni pale fedha inapotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali lakini haifiki kwa wakati.

"Azimio letu tunataka fedha zilizotengwa ziende kwa ajili ya ujenzi wa barabara nchini hata kama si zote, kwa maana tunaenda robo ya pili ya bajeti lakini imekwenda asilimia 12 pekee, imebaki mwezi mmoja kujadili bajeti inayofuata. Naona fedha zipelekwe haraka," alisema.

Akichangia hoja hiyo, Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, alisema suala la barabara nchini ni mtandao muhimu na kwamba katika bajeti TANROADS iliomba Sh. trilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa barabara lakini imepewa Sh. trilioni 1.5 tu.

Alisema mkoa wa Mbeya wananchi wanashindwa kupeleka mazao sokoni kutokana na ubovu wa miundombinu ya baadhi ya barabara.

"Tunaomba wizara husika ya fedha ambayo iliahidi kupeleka fedha kwa wakati ingeshapeleka, tusiongee kisiasa kwamba tutapeleka kabla ya kumaliza bunge mkutano unaisha kesho na Wabunge wa majimbo wanasema hazijapelekwa tunaomba Spika kiti chako kitoe onyo kali fedha zipelekwe," alisema.

Mbunge wa Kibamba (CCM), Issa Mtemvu, alisema mvua inayoendelea imeharibu miundombinu mkoani Dar es Salaam na wananchi wanashindwa kutoka kuendelea na shughuli za kiuchumi. "Katika kipindi cha miaka miwili kwa sasa hakuna fedha zozote zimekuja kusaidia mtandao wa zaidi ya kilomita 144,000 nchini zinazosimamiwa na TARURA. Hali ya barabara ni mbaya sana," alisema.

Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema hali ya barabara ni mbaya na maeneo mengi hayapitiki hasa ya vijijini. Mfano, alisema mkoani Mtwara, Mto Lukuledi umefurika na kuomba serikali itoe fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo.

Mbunge wa Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya, alisema barabara za vijijini zina hali mbaya huku akitolea mfano eneo la Lipalamba kulikuwa na daraja ambalo limekatika hali iliyosababisha mama mjamzito kujifungulia njiani kwa sababu ya kushindwa kupita.

**BIL.200/- ZINAHITAJIKA**

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema mvua ya El Nino imeharibu barabara na madaraja baadhi ya maeneo nchini na serikali imeendelea kuchukua hatua. "Dosari zimekuwa kubwa, wizara tumefanya tathmini ya athari ya mvua mikoa yote na kubainisha hasara ya Sh.Bilioni 200 imetokana na kuharibika kwa barabara na madaraja,"alisema.



Wapita njia wakishuhudia ubovu wa barabara ya Nangurukuru hadi Liwale, eneo la Mlowoka, mkoani Lindi juzi, ambayo imeharibika kutoka na mvua zinazonyesha mkoani humo. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi vijana wapewa 'nondo kuhusu Lowassa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro, Joseph Masunga, amesema viongozi vijana wana mambo mengi ya kujifunza na kuiga kutoka kwa Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Lowassa, kutokana na mambo aliyoyafanya katika kusimamia maendeleo nchini.

Alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari na kusema Lowassa alikuwa kiongozi makini, jasiri, shupavu, asiyeogopa kutoa maamuzi yenye maslahi kwa Taifa.

Pia alisema Lowassa alikuwa mahiri na mwenye uthubutu mwenye kariba za uongozi ambazo vijana wanapaswa kuwa nazo.

Masunga alisema Lowassa alisimamia na kufuatilia mambo mengi ambayo yalileta matokeo mazuri ikiwamo kampuni ya City Water iliyopewa kazi ya kusimamia usambazaji wa huduma ya maji Dar es Salaam.

Baada ya kampuni hiyo kushindwa kuwajibika, huku ikiwa na uwezo mdogo, Lowassa, wakati huo akiwa Waziri wa Maji na Mifugo, alichukua uamuzi wa kuvunjwa kwa mkataba wake.

Alisema Lowassa alisimamia kwa ukamilifu katika kila eneo alilopewa kutekeleza wajibu wake na kufuatilia, akitoa maelekezo alihakikisha hayaishii njiani, hivyo ataendelea kukumbukwa kwa mchango wake.

Pia alisema akiwa Waziri wa Ardhi Lowassa alifanikisha kurejesha eneo la Mnazi Mmoja baada ya kuwafukuza wavamizi wakitaka kujenga bila kufuata taratibu za sheria za ardhi.

Mhandisi Masunga alisema Lowassa alisimamia na kufuatilia na kuleta matokeo mazuri kwenye mgogoro uliokuwapo kati ya mataifa ya Misri walioona wana mamlaka zaidi ya kutumia maji ya Ziwa Victoria kuliko Watanzania kwa kutumia mikataba iliyosainiwa enzi za ukoloni.

Mhandisi Masunga Lowassa pia alisimamia suala la elimu nchini na kuhakikisha shule za sekondari za kata zinaanza kujengwa kwa kasi jambo lililosaidia kwa sasa wanafunzi wote wanaendelea na elimu ya sekondari nchini.

## Watalii wa ndani waongezeka Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

IDADI ya watalii wa ndani wakiwamo kutoka Tanzania Bara imeongezeka visiwani hapa hadi kufikia milioni 1. 5 katika kipindi cha mwaka 2023.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Fatma Mbarouk Khamis.

Fatma alisema idadi hiyo imeongezeka kutoka watalii 530,000 waliotembelea vivutio vya utalii visiwani hapa kwa miaka iliyopita.

Akizungumza na waandishi wa habari kuelekea Tamasha la Utalii Zanzibar, alisema kuongezeka kwa idadi hiyo ya watalii hao wa ndani ni moja ya mafanikio ya sekta hiyo hasa kuanzia kwa wenyeji wenyewe.

"Kwa mwaka 2023 katika utalii wa ndani tuseme tumevuka lengo, watalii ni wengi wamejitokeza kutoka mikoa ya Tanzania Bara, pia idadi ya mikutano inayofanyika hapa kutokea bara ni mingi siku hadi siku, haya ni mafanikio," alisema.

Fatma, alisema lengo la Serikali ya Zanzibar kupitia wizara hiyo kwa mwaka huu ni kuongeza watalii hadi kufikia 700,000 kutoka mataifa mabalimbali duniani.

Kuhusu tamasha hilo lililoandaliwa na Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI) kwa kushirikiana na Kampuni ya Kili Fair, alisema ni la pili kwa mwaka huu, litafanyika kuanzia Februari 21 hadi 22, mwaka huu, visiwani hapa.

Alisema matamasha kama hayo yana mchango mkubwa kutangaza vivutio vya utalii nchini kupitia bidhaa zinatengenezwa Zanzibar kwa watalii wa ndani na nje ya nchi.

Katibu Mkuu alisema utalii umesaidia kuinua sekta za maendeleo, utunzaji mazingira, kuitangaza Zanzibar kupitia vivutio vyake na kutoa ajira kwa wananchi.

Makamu Mwenyekiti wa ZATI Zanzibar, Clara Riera, alisema lengo la tamasha hilo ni kuwaunganisha wadau wa utalii kutoka maeneo mbalimbali.

Alisema tamasha hilo pia litasaidia kuitangaza tamaduni za kizanzibari na kuinua uchumi wa Zanzibar.

Mkurugenzi wa Kili Fair, Dominic Shoo, alisema wawekezaji kutoka nchi 25 za Afrika Mashariki Asia na Ulaya wanatarajia kushiriki katika tamasha hilo.

# Mahakama yaelezwa wakili feki alivyonaswa

**Na Grace Gurisha**

OFISA wa Polisi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Kanda Maalum ya Dar es Salaam (ZCO), Inspekta Sultan Mohamed, ameieleza mahakama kuwa mshtakiwa Baraka Mkama alipohojiwa alitaja namba yake ya uwakili kuwa ni 4696 lakini ilipoingizwa kwenye mfumo likatokea jina la mtu mwingine ambaye anadaiwa kuwa ni Mwalimu wa Chuo Kikuu Dodoma.

Aidha, amedai kuwa wakili huyo feki alikamatwa katika viwanja vya mahakama hiyo Mei 23, 2023 baada ya kuzuia askari kutowakamata washtakiwa ambao kesi yao iliondolewa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya, kwa madai kuwa yeye ni wakili wao.

Ofisa huyo alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ushindi Swalo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati akitoa ushahidi katika kesi dhidi ya Mkama anayedaiwa kujifanya ni wakili wakati akijua si kweli.

Alidai kuwa Mei 23, 2023 muda wa mchana, akiwa ofisi ya polisi ndani ya jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, alisikia kelele za watu zikitokea geti la kuingilia mahakamani hapo.

"Nilienda getini na kumkuta askari Mbaraka akiwa ameshikana na mtu mwanamume aliyevalia suti nyeusi na skafu ya uwakili wa kujitegemea huku askari huyo akiwa amechubuka mkononi kwenye kiwiko," alidai.

Mohamed alidai kuwa kutokana na hali hiyo, alitumia busara kuwatuliza na kuwataka waende ofisini na kumuuliza askari kilichotokea na kumwambia kuwa mtu huyo alimzuia kukamata washtakiwa ambao kesi yao iliondolewa mbele ya Hakimu Mbuya.

"Wakati anataka kuwakamata mtu huyo aliyejitambilisha kama wakili wao, alimzuia kuwakamata ndani ya jengo na alimshambulia. Nilimhoji mtu huyo na akajitambulisha kuwa yeye ni wakili wa washtakiwa hao na ni mwanachama wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS),"alidai.

Inspekta Mohamed alidai kwamba aliwapigia simu viongozi wake katika ofisi ya ZCO na walifika akiwamo Sajenti Stefano na gari na kumchukua mshtakiwa hadi kituo kikuu (central) kwa mahojiano zaidi.

"Akiwa bado yuko ofisi ya polisi katika Mahakama Kisutu, alifika mwakilishi kutoka TLS ambapo walikwenda wote ofisi ya ZCO alikopelekwa. Mshtakiwa alipohojiwa alitaja namba yake ya uwakili kuwa ni 4696. Baada ya hapo mwakilishi wa TLS aliingiza namba hiyo katika mfumo na likatoka jina la mtu mwingine ambaye anadaiwa kuwa ni mwalimu," alidai.

Baada ya kueleza hayo, mshtakiwa alipopewa nafasi ya kumhoji shahidi huyo hakuwa na swali lolote dhidi yake.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 11, 2024 kwa mashahidi wa upande wa mashtaka kuendelea kutoa ushahidi wao.



Mkurugenzi wa jumuiya ya waandishi wa habari za mazingira Tanzania, John Chikomo (kushoto), akizungumza na baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki mafunzo ya uhifadhi wa mazingira, yaliyoandaliwa na jumuiya hiyo kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi mali asili, mjini Bagamoyo mkoani Pwani jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kigezo vyeti JKT, JKU ajira chaondolewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeondoa kigezo cha cheti cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa vijana wote kupewa fursa sawa katika ajira pale wanapokuwa wametimiza masharti mengine yanayohusika na nafasi ya ajira husika.

Akisoma azimio hilo bungeni jana, Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, alisema: "Kwa kuwa Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi hawana uwezo wa kuwapokea na kumudu vijana wote wanaohitimu kidato cha nne na sita."

"Na kwa kuwa upo uwezekano wa vyombo vya ulinzi na usalama kuwapeleka JKT na JKU vijana watakaokuwa wameajiriwa kukidhi masharti ya msingi ya ajira husika na kwa kuwa wapo vijana wenye sifa uwezo wanaoweza kutimiza masharti ya ajira kwenye vyombo vya ulinzi na usalama isipokuwa sharti la kupitia mafunzo ya JKT na JKU."

Alisema Bunge linaazimia vijana wote wapewe fursa sawa katika ajira pale ambapo wanakuwa wametimiza masharti mengine yote yanayohusika na nafasi ya ajira husika isipokuwa cheti cha JKT na JKU hadi pale ambapo serikali itakapokuwa na uwezo wa kuwapokea na kuwapa mafunzo ya JKT na JKU vijana wote wanaohitimu kidato cha nne na cha sita.

Hatua hiyo ya Bunge imetokana na hoja ya dharura ya Mbunge wa Mbozi (CCM), George Mwenisongole, kuomba bunge lijadili kigezo kilichowekwa cha lazima mwombaji awe amepitia JKT katika ajira zilizotangazwa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama.

Katika maelezo yake, mbunge huyo alisema kuna wanafunzi wanamaliza kidato cha nne takribani 500,000 wanaomaliza kidato cha sita takribani 200,000 na kuna wanaomaliza darasa la saba milioni moja na wote wangependa kupata nafasi ya kuajiriwa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama.

"Kwa sababu kwa sasa jeshi letu halina uwezo wa kumchukua kila mwanafunzi na wanaopata nafasi ni wachache na ndio wanaopata nafasi ya kuajiriwa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, naomba kutoa hoja kigezo hiki kiondolewe," alisema.

Akichangia hoja hiyo, Mbunge wa Viti Maalum, Felister Njau, alisema vijana wengi wanaachwa na kuna mgawanyiko wa usawa na kwamba pamoja na majeshi kutumia kigezo cha JKT na JKU, taasisi zingine zimeiga na kusababisha wengine kutoajirika.

Alishauri vijana wasailiwe na watakaofaulu taasisi husika ichukue jukumu la kuwapeleka kwenye mafunzo kama kigezo kitakuwa hicho.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christine Mzava, alisema kigezo kinachowekwa ni ubaguzi kwa sababu nchi imejenga shule nyingi za kata wengi wanasoma wanahitimu lakini inapofika suala la kuwaajiri JKT inakuwa kigezo.

Mbunge wa Sengerema (CCM), Hamis Tabasamu, alishauri kutenga bajeti kubwa ili kuruhusu vijana wote kwenda kwenye mafunzo huku Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko, akisema vigezo vinavyotumika ni dhambi kuwabagua kwa kuajiri wengine kwa kutumia kigezo cha kupitia JKT, hivyo bunge lisikubali.

Mbunge wa Viti Maalum, Ag-

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi Ligi Kuu Bara wanahitaji mafunzo zaidi

**WAKATI** mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu Tanzania Bara umeanza, bado kumekuwa na malalamiko mbalimbali kutoka kwa wadau wa mchezo wa kandanda kuhusiana na uchezeshaji wa mechi za ligi hiyo.

Waamuzi wamekuwa wakitoa maamuzi tata katika mechi wanazochezesha ambazo baadhi ya timu hunufaika huku nyingine zikiumia kutokana na maamuzi yanayotolewa.

Huku mzunguko wa pili ukiwa unaanza leo kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro kwa mabingwa watetezi kuwavaa wenyeji KMC, tayari kila timu inafahamu inahitaji kufikia malengo gani pale msimu utakapokamilika.

Zipo timu ambazo zinaamini zinaweza kupambana kutwaa ubingwa wa ligi hiyo na kupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye mashindano ya kimataifa na nyingine zikiwa na lengo la kumaliza kwenye nafasi nne za juu.

Pia kuna timu ambazo sasa tayari zinahitaji kupambana kuhakikisha zinavuna pointi muhimu na kujiona katika hatari ya kushuka daraja na zinaamini hakuna kinachoshindikana endapo juhudi, kujitoa na kucheza kwa nidhamu kutachukua nafasi yake.

Lakini pia tunafahamu zipo timu ambazo zinaamini ziko mahali salama na zinashuka dimbani bila presha yoyote, hawa mwisho wa siku hushangaza wadau kwa sababu wanaweza kumaliza juu au wakaburuza mkia na kushangaa jambo hilo limewafikaje wao.

Mpira ni mchezo wa hadharani, vile vile waamuzi kazi yao huonekana na endapo wanafanya vibaya au kinyume na sheria zinazowaongoza, kuna kila sababu ya nchi kupata bingwa ambaye hastahili kutokana na 'kubebwa'.

Katika kuhakikisha thamani na hadhi ya Ligi Kuu Tanzania inaendelea kupanda, muda umefika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Kamati ya Waamuzi wakawaandalia upya mafunzo waamuzi wetu ili kutekeleza majukumu yao katika ubora.

Mafunzo ndio njia sahihi ya kuwaimarisha waamuzi wetu ambao tunaamini viwango vyao vikiimarika, tutawashuhudia wakisimamia michezo mbalimbali ya kimataifa kama Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambazo zimemalizika wikendi iliyopita kwa wenyeji, Ivory Coast kutwaa ubingwa.

Lakini pia waamuzi wenyewe wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake Nchini, wakati wote mnatakiwa kupitia mafunzo yenu na kujikumbusha ili kupunguza au kumaliza 'maboko' yanayowashushia heshima yenu.

Kujikumbusha kanuni na kupitia mechi nyingine za ligi zilizoendelea ndio jambo mnalotakiwa kulifanya na kwa namna hiyo kutawasaidia mtekeleze majukumu yenu vizuri na 'kuwasuta' wale wanaowatuhumu mnatoa maamuzi mbalimbali kwa nguvu ya 'bahasha' kutoka kwa timu za wapinzani.

Mbali na mafunzo, TFF inatakiwa pia kuongeza adhabu kwa waamuzi wanaoshindwa kutafsiri vyema sheria za mchezo huo wenye mashabiki wengi nchini kwa sababu makosa wanayofanya yanaumiza na hayalingani na adhabu inayotolewa.


Adhabu zinapokuwa kubwa, huenda zikawafanya waamuzi kuongeza umakini na hatimaye kuchezesha kwa haki, lakini pia haitaleta unyonge kwa upande wowote kwa sababu idadi kubwa ya makosa huzikuta timu zenye majina madogo huku faida ikienda kwa klabu kongwe.

Kila timu imefanya usajili mzuri pamoja na kuboresha mabenchi ya ufundi kwa sababu inataka kuvuna matokeo chanya katika mechi zake na si vinginevyo.

Kwa ujumla tunapenda kushuhudia kila timu ikivuna kile inachostahili na si kila siku makosa ya kibinadamu kuonekana kuwafaidisha 'vigogo' na kuleta tafsiri mbaya.

Bila kusahau tunawakumbusha wachezaji, viongozi, mashabiki na wadau wa soka kuonyesha nidhamu wakati timu zenu pendwa zinapokuwa uwanjani kusaka pointi muhimu na vile vile kutowadhalilisha waamuzi wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Bodi Ligi Kuu ikikutana mapema huleta maana

**MARA** kwa mara, wadau, waandishi wa habari na wachambuzi wa soka wamekuwa wakielezea umuhimu wa Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) kutoa maamuzi yao mapema.

Wamekuwa wakieleza faida ya maamuzi ya mechi mbalimbali za Ligi Kuu kutolewa mapema, lakini pia kuzifanya adhabu kuonekana ni adhabu kweli na si mapumziko ya mechi.

Tumeshuhudia baadhi ya wachezaji wakifanya makosa, lakini zinapita mechi tatu au nne, tena wakati mwingine zile muhimu, baada ya hapo mchezaji anafungiwa mechi tatu katika mechi ambazo si zenye presha sana katika timu yake.

Wala si mara moja ama mbili tumeona kamati ikishindwa kutoa adhabu kwa wachezaji wa Simba, au wa Yanga kwa sababu kuna mechi kubwa za 'dabi'. Wanasubiri mpaka zipite ndiyo wanakutana na kutoa adhabu.

Najua kabisa kamati hiyo inafahamu maana ya adhabu, iwe kwenye nyanja ya soka, kazini au kifamilia.

Hutolewa ili aliyetenda kosa aumie, ajutie, nafsi yake ione au ihisi joto la adhabu iliyotolewa ili ajifunze au kujirekebisha kutofanya hivyo tena.

Sasa kama mchezaji anatafutiwa mechi gani akae na acheze, hiyo haina sifa ya kuwa adhabu. Ni kitu kingine kabisa.

Uharaka wa kukaa vikao vya kamati hiyo nao unatakiwa, angalau mara mbili kwa mwezi.

Hii inafanya aliyepata adhabu au aliyeonewa kupata hali yake kwa muda muafaka.

Wataalam wa sheria wanasema haki ikitolewa au ikitendeka siyo itendeke tu, ila ionekane imetendeka.

Binafsi nimefurahishwa sana na uharaka na kamati hiyo kumfutia adhabu winga wa Tanzania Prisons, Zabona Mayombya.

Inawezekana tu ikawa kwa bahati, tukio limetokea wakati kamati ikiwa inajiandaa kukutana, lakini iwe hivyo au tofauti, imetuonyesha faida ya kufanya maamuzi kwa haraka.

Ni Jumapili tu iliyopita, mchezaji huyo alipigwa kadi nyekundu katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya dhidi ya Yanga, timu yake ikipoteza mabao 2-1.

Mwamuzi, Ahmed Aragija alimwonyesha mchezaji huyo kadi kwa madai alijiangusha ndani ya eneo la hatari alipokuwa akikokota mpira nyuma yake kukiwa na beki wa Yanga, Bakari Mwamnyeto.

Ilikuwa ni kadi ya pili ya njano, hivyo Mayombya alipaswa kuukosa mchezo unaofuata.

Siku tatu baadaye, kamati ilikaa na kutengua maamuzi hayo, ikifutilia mbali kadi hiyo na kusema ni kweli mchezaji huyo alisukumwa.

Uharaka huyo ukasababisha Mayombya kucheza mechi ya juzi dhidi ya Singida Fountain Gate na akafunga mabao mawili, akatoa pasi ya mwisho 'asisti' na kuisaidia timu yake, Prisons kushinda mabao 3-1 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Amefaidika na ameifaidisha timu yake kutokana na maamuzi yaliyotolewa muda mfupi tu baada ya tukio hilo.

Inafikirisha, kama angekaa kwa muda mrefu, labda mechi nne baada ya tukio, ina maana asingecheza mechi dhidi ya Singida, timu ya Prisons isingepata huduma yake, na inawezekana ingeweza kufungwa bao 1-0.

Na inawezekana asingecheza hizo mechi asingekuwa na utimamu wa mwili, hivyo asingeweza kufanya vizuri katike mechi ya mwanzo kama alivyofanya dhidi ya Singida Fountain Gate.

Kwa maana hiyo tunaishauri kamati hiyo iwe inafanya haraka kukutana kwa ajili ya kupitia baadhi ya mechi za Ligi Kuu kwa haraka ili kila mmoja apate haki yake bila kuchelewa.

# Kipenga uchaguzi udiwani kata 23

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetangaza uchaguzi mdogo wa madiwani kwenye kata 23 za Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Kailima Ramadhani, jijini Dodoma jana, uchaguzi huo utafanyika Machi 20, mwaka huu.

"Fomu za uteuzi zitatolewa kuanzia Februari 26 hadi Machi 4. Uteuzi wa wagombea utafanyika Machi 4, 2024 na kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia machi 5 hadi 19, 2024," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo iliainisha kuwa uchaguzi huo umetangazwa kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, akiiarifu tume kuhusu uwapo wa nafasi wazi za madiwani katika kata 23 za Tanzania Bara.

Taarifa iliongeza kuwa waziri ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

"Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya tume katika kipindi cha uchaguzi huu mdogo," ilisisitiza taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kata zitakazofanya uchaguzi huo mdogo na halmashauri zilizoko katika mabano ni Kimbiji (Manispaa ya Kigamboni), Kasingirima (Manispaa ya Kigoma/Ujiji), Ndevelwa (Manispaa ya Tabora) na Msangani (Mji Kibaha).

Zingine ni Fukayosi (Bagamoyo), Mlanzi (Kibiti), Utiri (Mji Mbinga), Mbingamhalule (Songea), Isebya (Mbogwe), Kibata (Kilwa), Mshikamano (Wilaya Musoma), Busegwe (Butiama), Nkokwa (Kyela) na Kamwene (Mlimba).

Pia zimo Chipuputa (Nanyumbu) na Buzilasoga (Sengerema), Mhande (Kwimba), Kabwe (Nkasi), Bukundi (Meatu) Mkuzi (Muheza) na Boma, Mtimbwani na Mayomboni (Mkinga).

# Majaliwa akoleza moto ushiriki wanawake kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amewataka viongozi wa Serikali na sekta binafsi waweke mikakati ya kuwashirikisha kikamilifu wanawake katika fursa za uchumi wa kidijitali ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Majaliwa aliyasema hayo juzi alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kufungua mkutano wa Future Ready Summit jijini Dar es Salaam.

"Viongozi wa serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi wekeni mikakati ya pamoja ya kukuza ushirikiano na kuwekeza kwenye miundombinu ya TEHAMA (teknolojia ya habari na mawasiliano) ili kutoa kipaumbele katika kuongeza ujumuishi wa kidijitali na wa kifedha," alisema.

Katika mkutano huo ulioandaliwa na kampuni ya Vodacom, Waziri Mkuu ametoa wito kwa kampuni za simu yaweke gharama rafiki za mawasiliano ili kuvutia washiriki wengi wakiwamo wanawake kushiriki katika fursa za uchumi wa kidijitali.

Pia aliwataka wadau wa sekta binafsi, watumie majukwaa kama hilo la Future Ready Summit pamoja na kuandaa programu za kuwawezesha vijana, hususan wakike ili nao waweze kushiriki katika kuchangia uchumi wa taifa.

"Kwenu washiriki wa mafunzo tumieni fursa hii vyema, shirikianeni na wawezeshaji, muwe na mijadala yenye tija ili mafunzo yawe na tija inayotarajiwa. Aidha, mkawe mabalozi wazuri kwa wasichana na wanawake kuhusu fursa zakidijitali na matumizi ya TEHAMA," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa shule za sekondari 26 za kitaifa za wasichana mahsusi kwa masomo ya sayansi ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuwachochea wanafunzi wa kike wapende masomo hayo.

Alisema shule hizo zinajengwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa gharama ya shilingi bilioni 104 ambapo ujenzi wa kila shule moja inagharimu kiasi cha shilingi bilioni nne.

"Katika hili ninampongeza sana Rais Samia ambaye ni kinara wa kuhamasisha masuala ya sayansi, teknolojia na hisabati. Hii ni kutokana na utashi wake na hatua za makusudi alizozichukua kuhakikisha wasichana wanashiriki kikamilifu katika fursa za masomo ya sayansi na hisabati," alisema.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliwaondoa hofu Watanzania juu ya mapinduzi ya teknolojia na kuwataka wajipange na wasonge mbele.

Pia alisema jukumu la wizara hiyo ni kuhakikisha uwekezaji unafanyika kwenye ujenzi wa miundombinu ya taasisi na vyuo ambavyo vitafundisha masomo hayo. Alisisitiza kuwa Tanzania iko tayari kwenda mbele katika mapinduzi ya kiteknolojia.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (wa pili kulia), akifurahia jambo na Maofisa Waandamizi wa kampuni za Dough Works Ltd na Oryx Ernegies Tanzania baada ya kuzindua mgahawa mpya wa KFC Magomeni, Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Dough Works, Vikram Desai. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# SMZ yakiri bei juu bidhaa toka nje

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara, Maendeleo ya Viwanda Zanzibar imekiri kuwepo kwa upandaji wa bei za bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka nchi za nje.

Amesema hali hiyo inatokana na sababu tofauti zikiwemo za upungufu wa baadhi ya bidhaa katika masoko ya nje.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Biashara, Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Jimbo la Paje, Dk. Soud Nahoda.

Mwakilishi huyo alihoji upandishaji wa bei ya vyakula na bidhaa kiholela akisema umekuwa ni tatizo kubwa visiwani hapa na kuongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wenye kipato cha chini, akihoji lini litatatuliwa tatizo hilo.

Akijibu swali hilo, Waziri Omar alisema sababu nyingine ni kupanda kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa kwa baadhi ya nchi na gharama za kubadilishia fedha za kigeni na kusababisha kuadimika kwa bidhaa hizo nchini.

Omar alisema serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda pamoja na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara ina utaratibu wa kufanya mapitio ya bei elekezi za bidhaa kwa zile zinazodhibitiwa pale inapohitajika kufanya hivyo.

"Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara Namba 5 ya Mwaka 2018 Kifungu Namba 5 (c) na 61 kinatoa mamlaka ya kupanga na kusimamia bei elekezi kwa bidhaa zinazodhibitiwa na Serikali kila panapokuwa na mfumko wa bei usiokuwa na sababu kwenye soko"alisema.

Alisema Wizara ya Biashara huwa inatangaza bei hizo kila panapotokea mabadiliko ya bidhaa hizo na suala hilo litapungua iwapo uzalishaji wa bidhaa muhimu utaongezeka.

# Bunge lataka udhibiti gharama matibabu

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

BUNGE limeazimia serikali kuanzisha mfumo thabiti utakaounganisha bodi zote zinazosimamia gharama za huduma za afya katika vituo vya afya vya binafsi na vya hiari.

Azimio hilo lilitolewa juzi baada ya kubainika uwapo wa gharama tofauti za huduma za afya bila kuwapo bei elekezi katika huduma zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya.

Kwa kufanya hivyo, ilielezwa kuwa thamani halisi ya fedha za umma inayotumika kwenye usimamizi na udhibiti wa vituo hivyo, itakuwa imepatikana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Nanghwenja Kaboyoka, wakati anawasilisha taarifa ya shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2023, alisema mapendekezo hayo yanatokana na uchambuzi wao katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema uchambuzi wa kamati katika taarifa ya CAG kuhusu udhibiti wa vituo hivyo, umebainisha upungufu katika udhibiti na usimamizi madhubuti wa vituo hivyo katika maeneo ya usajili, usimamizi shirikishi, ukaguzi, tathmini za huduma na udhibiti wa bei.

Dosari hizo, alisema zimesababisha vituo hivyo kutokutoa huduma bora za afya ambazo zinatarajiwa kutolewa na vituo vya afya binafsi na hiari, ambayo imechangiwa na kuwapo kwa mwingiliano wa majukumu ya bodi na mabaraza ya usimamizi wa huduma ya afya.

Pia alisema upungufu huo unachangia kutopatikana thamani halisi ya fedha za umma zinazoelekezwa kwenye vyombo vya udhibiti wa huduma za afya hapa nchini. Katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa vituo vya afya vya binafsi na vya hiari, Mwenyekiti huyo alisema ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Afya haikuhakikisha kuwa bei za matibabu zinawekwa wazi kwenye baadhi ya vituo vya afya vya binafsi na vya hiari.

Aidha, alisema ilibainika kuwa bei za huduma za afya zilitofautiana kwenye vituo vya afya vya binafsi na hiari katika mikoa yote.

Alisema matokeo ya ukaguzi wa kiwango cha nyota cha vituo vya afya vya binafsi 518, kati ya vituo 1474 uligundua, ni asilimia 18 tu iliyofikia kiwango cha nyota tatu, na zaidi mpaka kufikia Juni 2022.

Kutokana na hali hiyo, alisema wizara haikufikia malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara (2016/17-2020/21), unaobainisha kuwa Wizara ya Afya ilipanga kufikia ubora wa vituo vya afya



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (kulia), akizungumza na wananchi wa Utegi wilayani Rorya juzi, alipofanya ziara ya kusikiliza kero zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazalishaji unga wafundwa kuepuka sumukuvu

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Nchini (TBS), limewataka wazalishaji unga na karanga kuzingatia na kuimarisha usalama wa bidhaa zao ili kulinda afya za walaji dhidi ya sumu kuvu.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Dk. Athumani Ngenya, alisema hayo juzi wakati akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo kwa wadau wa unga wa mahindi, unga mchanganyiko, siagi na karanga.

Alisema chakula ni hitaji muhimu kwa maisha ya binadamu, ustawi na maendeleo ya nchi hivyo umuhimu, usalama na ubora wa chakula lazima upewe kipaumbele katika kulinda afya ya jamii na uchumi wa nchi na kuwa kigezo muhimu katika biashara ya kitaifa na kimataifa.

"Chakula kisipokuwa salama husababisha madhara ya kiafya na hata vifo kwa walaji sanjari na athari za kiuchumi chakula kisipokuwa salama husababisha madhara ya kiafya na hata vifo kwa walaji sanjari na athari za kiuchumi," alisema.

Dk. Nyenya alsiema azma ya serikali ni kujenga uchumi imara na endelevu, wenye nguvu na ushindani kwa kuvutia uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara hivyo usalama wa chakula lazima uzingatiwe ili kufikia malengo hayo.

Alisema katika kuunga mkono mipango na juhudi zote zinazofanywa na serikali, TBS inawajibika kikamilifu kuhakikisha kuwa chakula pamoja na bidhaa nyingine zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazotoka nje ya nchi zinakidhi matakwa ya viwango kwa lengo la kulinda afya ya jamii.

"Sote tunatambua kuwa bidhaa zitokanazo na nafaka husan unga pamoja na bidhaa za karanga ni mojawapo ya vyakula vinavyotumika kwa wingi hapa nchini hivyo basi, endapo bidhaa hizo hazitakidhi matakwa ya usalama na ubora huweza kusababisha madhara ya kiafya na kiuchumi," alisema.

Kwa mantiki hiyo, alisema TBS itaendelea kutilia mkazo suala la usimamizi wa viwango na kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa hizo pamoja na aina nyingine za bidhaa za vyakula.

Alisema TBS inatambua umuhimu wa bidhaa zitokanazo na nafaka hususan unga wa mahindi na nafaka nyinginezo pamoja na bidhaa zitokanazo na karanga na ndiyo sababu imeandaa mkutano huo mahsusi kwa ajili ya wazalishaji wa bidhaa hizo.

"Ninapenda kutoa rai kwenu kuzingatia kikamilifu elimu itakayotolewa na wataalam wetu ili kuendelea kuimarisha usalama na ubora wa bidhaa za unga wa mahindi na nafaka nyinginezo, unga mchanganyiko pamoja na bidhaa za karanga kwa kukabiliana na vihatarishi mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa sumukuvu," alisema.

Alisema bidhaa za karanga zinao uwezekano mkubwa wa kuchafuliwa na sumukuvu na kuathiri usalama wake endapo kanuni bora za kilimo, uhifadhi, usafi, usafirishaji, usindikaji na uandaajihazitazingatiwa kikamilifu katika mnyororo wa thamani.

TBS, alisema imekuwa ikitoa mafunzo ya aina hiyo mara kwa mara ili kuwakumbusha kuhusu, sheria, kanuni na taratibu za kuzingatiwa wakati wa kutengeneza na kusambaza bidhaa za chakula.

Alisema iwapo chakula kikipimwa kwenye maabara za TBS na kupitishwa zinakuwa na ubora kwenye masoko mbalimbali Afrika Mashariki na kwingineko hivyo mfanyabiashara anakuwa na uhakika wa soko.

Baraka Nyirenda mzalishaji unga kutoka mkoa wa Songwe, alisema mafunzo hayo yamekuwa msaada mkubwa kwa wafanyabiashara kuzingatia ubora hali ambayo inawawezesha kupata masoko kwa urahisi.

"Hii ni fursa kwetu kuongeza ubora kwenye uzalishaji kwasababu ukizalisha bidhaa na ikapimwa TBS ikaonekana imekidhi viwango inaweza kuuzwa kwenye soko lolote duniani cha muhimu ni kuzalisha kwa ubora unaotakiwa," alisema.

# Wadudu washambulia ekari 2,500 za viazi

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

WADUDU wasiofahamika wamevamia mashamba na kuharibu ekari zaidi ya 2,500 za viazi mviringo katika kata sita wilayani hapa mkoa wa Njombe.

Hali hiyo imezua malalamiko kwa wakulima kutokana na kutokuwepo kwa kiuatilifu ambacho kimethibitika kuwa na uwezo wa kuwaua na kudhibiti kusambaa mashambani na kuzuka hofu ya kukosa mavuno ya kutosha na kuporomoka kwa uchumi miongoni mwao.

Mmoja wa wakulima hao, Ackson Mbogela, alisema wadudu hao wanakula majani, maua na viazi ambavyo vimeanza kukomaa.

"Ukipita mashambani unaona mashina tu, hakuna majani wala maua, kuna uwezekano tusipate mavuno, tumejaribu kutumia dawa mbalimbali, lakini wadudu hawa hawafi," alisema Mbogela.

Akim Aloyce, aliiomba serikali kuwapelekea wataalamu kufanya utafiti ili kubaini aina ya wadudu hao na kuwashauri aina ya viuatilifu vinavyoweza kutumika kuwaangamiza.

Alisema kwa sasa wadudu hao wameanza kuharibu viazi ambavyo vimeanza kuzaa baada ya kupukutisha majani na maua, hivyo kuna uwezekano wakapata mavuno kidogo au kukosa endapo hawatadhibitiwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alizitaja kata zilizoathiriwa na wadudu hao kuwa ni Ikuwo, Kigala, Itundu, Mlondwe, Matamba na Kinyika.

Mkufwe, alisema wanaendelea kufuatilia maeneo mengine ambayo mashamba ya viazi hayajavamiwa na wadudu hao na kuanza kukabiliana nao.

Aliwataka wakulima wa maeneo yote ya wilaya hiyo kuendelea kuzingatia ushauri wa wataalamu ili kukabiliana na uharibifu huo ambao unaendelea kutokea.

"Uharibifu huu ni mkubwa sana, tathimini tuliyoifanya inaonyesha ekari zaidi ya 2,500 ndizo zimeathirika, lakini tunaendelea kufuatilia na tunawashauri wananchi waendelee kuchukua hatua ili kupunguza hasara," alisema Makufwe.

Watafiti wa Kilimo wa Kituo cha Uyole jijini Mbeya wameweka kambi katika wilaya hiyo kufanya utafiti ili kubaini aina ya wadudu hao na kuanza kuwadhibiti.

Kiongozi wa Jopo la watafiti hao, Dk. Dora Mende, alisema watahakikisha wanatambua aina ya wadudu hao na dawa za kuwaangamiza.

Alisema aina ya wadudu hao hawajawahi kuwaona, hivyo wanaendelea kufanya utafiti.

Mkuu wa Idara ya Kilimo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Anincent Ndunguru, alisema wameanza kuchukua hatua za awali kwa kusambaza baadhi ya viuatilifu ambavyo wamepatiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Viuatilifu na Afya ya Mimea nchini (TPHPA).

Alisema upuliziaji wa viuatilifu hivyo unafanywa na maofisa kilimo wa kata na vijiji kwa kushirikiana na wakulima na kwamba tayari ekari zote 2,500 zilizokuwa zimevamiwa zimefikiwa.

Alisema kwa sasa wanaendelea kupulizia viuatilifu kwenye mashamba mengine ambayo yako jirani na mashamba hayo.



# Wadau wajadili kuboresha mazingira ya wafanyakazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VYAMA vya waajiri na mashirika ya vyama vya wafanyakazi wameanza kujadili na kutoa maoni ya Tanzania kuridhia mikataba sita ya Shirika la Kimataifa la Kazi Duniani (ILO) na marekebisho madogo ya sheria za kazi ili kuboresha mazingira ya wafanyakazi nchini.

Akifungua kikao hicho juzi jijini hapa, Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Said Mabie, alisema mwaka 1983 Tanzania iliridhia mkataba wa ILO wa masuala ya kazi na ajira.

"Kutokana na matakwa ya mkataba huo Tanzania imekuwa na utaratibu mzuri wa kushirikiana na wadau wa utatu yaani vyama vya waajiri na mashirika ya vyama vya wafanyakazi.

" Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipokea kutoka Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar pendekezo la nchi kuridhia mkataba wa ILO namba 102 wa mwaka 1952 unaohusu viwango vya chini vya mafao ya hifadhi ya jamii," alisema.

Alisema vyama vya wafanyakazi kupitia Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA), vimekuwa vikihimiza na kuishauri Serikali kuridhia mikataba ya ILO hususani wafanyakazi wa majumbani namba 189 wa mwaka 2011.

"Ndugu washiriki itakumbukwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza Serikali kufanyia kazi maombi ya nchi kuridhia baadhi ya mikataba iliyokuwa inapendekezwa kutoka kwa wadau ikiwemo TUCTA.

"Hivyo Serikali iliunda timu ya wataalamu ikiongozwa na makatibu wakuu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar ili kuchambua mikataba hiyo na kuja mapendekezo la uridhiwaji wake, ninayo furaha kuwaeleza kamati hiyo ilikutana na kuja na mapendekezo ya kuridhia mikataba sita ya ILO, " alisema

Aliitaja mikataba hiyo kuwa ni wa hifadhi ya jamii, mafao ya wafanyakazi wanaopata majanga yatokanayo na kazi, sera ya ajira, usalama na afya mahali pa kazi.

Mwingine ni mfumo wa kuhamasisha usalama na afya mahala pa kazi na wa wafanyakazi wa majumbani.

Alisema Serikali kwa kushirikiana na TUCTA, ILO na mashirika ya maendeleo yamewezesha kufanyika kwa kikao hicho kwa lengo la kupokea maoni ya wadau wa Utatu ili hatua nyingine za uridhiaji ziendelee.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alisema wanatambua umuhimu wa kuboresha sheria za kazi ili kulinda maslahi ya wafanyakazi, hivyo mkutano huo ni moja ya hatua muhimu za kuridhia mikataba ya ILO.

Mwakilishi wa ILO, Edward Mosly, alisema makubaliano ya kuridhia mikataba hiyo ni sehemu ya kukuza na kuendeleza viwango vya kazi duniani.

# Wanafunzi watakiwa kuripoti ukatili wa kijinsia

**Na Peter Mkwavila** DODOMA

WANAFUNZI wa shule za msingi mkoani hapa wametakiwa kutoa taarifa Dawati la Jinsia na Watoto za ukatili wa kijinsia ili kutokomeza vitendo hivyo katika jamii.

Mkaguzi wa Jeshi la Polisi, Theresia Mdendemi wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Dodoma, alisema hayo wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Chamwino iliyopo Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Aliwataka wanafunzi hao kutosita kutoa taarifa kwa dawati hilo dhidi ya watu wanaowaamini pindi wanapowafanyia ukatili huo ndani ya saa 72 ili vyombo vya dola vipate ushahidi.

"Ushirikiano huo utawezesha mtuhumiwa kuuunganishwa kwa kosa alilofanya kwa ushahidi tutakaopata kutoka kwa waliotendewa kwenye mwili wao," alisema.

Koplo Edith Siwango kutoka Dawati hilo Wilaya ya Dodoma, aliwataka wazazi kutenga muda kuzungumza na watoto wao dhidi ya vitendo hivyo.

"Tupo hapa kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu na wazazi mlio hapa nawaomba mtenge muda wa kuzungumza na watoto wenu ili wawe wanaelewa kwani kuwachapa watoto siyo suluhisho, kuongea nao na kuwaelimisha ndiyo suluhu,"

"Kama unataka mtoto wako awe msikivu ongea nae, tusiwaachie walimu peke yao, tukiongea nao watatueleza changamoto zao," alisema Siwango.



Mbunge wa Viti Maalum, Riziki Lulida (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mlebe, wilayani Chamwino mkoani Dodoma jana, kuhusu umuhimu wa kupanda miti na kutunza mazingira wakati wa zoezi la upandaji miti 2,500 lililoandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira (MCCCO). **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wananchi wahimizwa kupikia gesi asilia

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WANANCHI wametakiwa kuacha matumizi ya kuni na mkaa kwa kupikia nishati mbadala ikiwemo gesi asilia ili kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko tabianchi nchini.

Mbunge wa Viti Maalum, Riziki Lulida alitoa ushauri huo juzi baada ya kushiriki upandaji miti 2,500 katika Shule ya Msingi Mlembe na zahanati ya kijiji hicho wilayani hapa Mkoa wa Dodoma.

Tukio hilo liliratibiwa na Taasisi isiyokuwa ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya kukabilian na mabadiliko tabianchi na uhifadhi wa mazingira mkoani hapa ya MCCCO.

Lulida, alisema dunia inakabiliwa na na athari za mabadilko tabianchi kutokana na watu kuharibu mazingira kwa kukata miti kwa ajili ya kupata kuni na mkaa.

"Niwaombe Watanzania kuachana na matumizi ya nishati ya mkaa kwa ajili ya kupikia na kutumia nishati mbadala ili kutunza mazingira hali ambayo itasadia kurudisha uoto wa asili na kupunguza ukame uliopo katika baadhi ya mikoa.

"Ukiwa kwenye ndege juu Mkoa wa Dodoma unaonekana ni jangwa sana na hii yote ni kutokana ukataji miti ovyo ambao umeharibu mazingira, " alisema Lulida

Alisema jitihada zinahitajika kwenye mikoa ambayo imegeuka jagwa kutokana na kukithiri kwa uharibu wa mazingira.

"Hivi sasa mikoa kama Dodoma, Singida na Arusha ukiwa kwenye ndege juu unaona maeneo yake ni jangwa, jitihada za upanadaji miti na kuitunza zinahitajika kuunga mkono juhudi za Serikali za mapambano dhidi ya athari za mabadiliko tabianchi," alisema

Alisema katika kubabiliana na tatizo hilo ataongoza wadau wa mazingira kupanda miti shule zote za Mkoa wa Dodoma ili kuunga juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kutunza mazingira tangu akiwa Makamu wa Rais mwaka 2017. Katibu wa Taasisi hiyo, Benard James, alisema wamepanga kila mwaka kupanda miti milioni moja katika maeneo ya Mkoa wa Dodoma ili kuunga mkono jitihada za Serikali kulinda mazingira.

"Leo hapa tumeleta miti 2,500 ambayo imepandwa katika eneo la shule na zahanati lakini hili litakuwa endelevu ili kuendeleza mapambano dhidi ya athari za mabadiliko tabianchi nchini, " alisema





# Wizara ya Kilimo yapambana na inzi waharibifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) kwa kushirikiana na wadau wengine, inaendelea na kupambana na inzi waharibifu wa matunda visiwani hapa.

Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo jana katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani, Mussa Foum, aliyetaka kujua jitihada zinazochukuliwa kukabiliana na nzi hao na funza wanaoharibu maembe kwa muda mrefu.

Shamata, alisema Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imetoa msaada wa kitaalamu, dawa na vifaa vya maabara kuendelea kupambana na wadudu hao.

Aliwataka wananchi na wakulima visiwani hapa kuendelea kutoa ushirikiano ili kudhibiti wadudu hao.

"Mheshimiwa Spika ili kuondokana na tatizo hili ni muhimu kwa wakulima kutoa ushirikiano kwa kuweka usafi kwenye mashamba na kufukia matunda yaliyoathirika jambo ambalo litapunguza athari ya mashambulizi kwa asilimia 50,"alisema.

Wakati huo huo; Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shabani Ali Othman amesema boti 205 zimetolewa kwa wakulima wa mwani, kati ya hizo 40 ni kwa Unguja na nyingine 165 Pemba.

Alisema boti hizo ni kati ya 500 zilizotengenezwa kwa ajili ya kugawa kwa wakulima wa mwani.

"Ugawaji wa boti hizi 500 unaendelea. Wastani wa Shilingi za Tanzania Bilioni 4.3 zilitumika kwa ajili ya kutengeneza," alisema.

Alikuwa akijibu swali la Mwakilishi wa Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe, aliyetaka kujua idadi ya boti zilizotolewa kwa wakulima wa mwani katika visiwa hivyo.

# ZEC yaandikisha wapiga kura 57,887 awamu ya kwanza

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imekamilisha uandikishaji wa wapiga kura 57,883 katika daftari awamu ya kwanza.

Mwenyekiti wa ZEC, Jaji George Joseph Kazi aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa tathmini ya uandikishaji wapiga kura wapya kwa mwaka 2023.

Alisema katika idadi ya walioandikishwa idadi ya wanawake ni kubwa ikilinganishwa na wanaume, kwamba wanawake walikuwa ni 31,440 na wanaume ni 26,443.

Jaji Kazi alisema ZEC inatarajia kuweka wazi orodha ya wapiga kura hao katika vituo vyote vilivyotumika kwa uandikishaji Unguja na Pemba kwa muda wa siku saba kuanzia Machi 1 hadi saba mwaka huu.

Aidha alisema kazi hiyo inafanyika kwa mujibu wa maelekezo ya Kifungu cha 19 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Namba 4 ya Mwaka 2018, ambayo inamtaka ofisa uandikishaji kutayarisha na kuweka wazi orodha ya wapiga kura walioandikishwa.

Alisema sambamba na uwekaji wa wazi wa orodha ya wapiga kura wapya, tume itaweka wazi orodha ya wapiga kura walioomba kuhamisha taarifa zao kutoka eneo moja kwenda lingine la uchaguzi.

"Madhumuni ya kufanya hivyo ni kutoa nafasi kwa mwombaji aliyeandikishwa kuwasilisha malalamiko ya kurekebisha taarifa zake, kuomba jina lake liingizwe katika orodha iwapo aliandikishwa lakini hakuorodheshwa au kuweka pingamizi dhidi ya taarifa za muombaji mwengine alie katika orodha"alisema.

Alisema kufanya hivyo kutawawezesha kujua kama taarifa zao zimo katika orodha au kujua iwapo taarifa zao zimenakiliwa kwa usahihi au kuweka pingamizi kwa wasio na sifa.

Hivyo aliwataka wadau wa uchaguzi na wananchi kuwahamasisha vijana walioomba kuandikishwa kwenda kuangalia taarifa zao, kwani kufika kwao vituoni kuangalia taarifa kutawahakikishia nafasi ya kuwemo katika daftari na kuwa wapiga kura.

Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarusi Faina, alisema wanatarajia kuandikisha wapiga kura wapya 162,606.

Akitoa tathmini ya uandishaji kiwilaya, Faina alisema wilaya ambayo imeandikisha watu kidogo ni Mkoani Pemba iliyoandikisha watu 2,562, lengo lilikuwa ni kuandikisha 11,964.

Wilaya nyingine ni Micheweni (2,628), lengo 10,907 Wilaya ya Magharibi A Unguja (7,157) lengo ni 28,677 Wilaya ya Kusini Unguja (2,875) lengo ni 4,792, Wilaya ya Kaskazini A unguja (7,265) lengo 13,169, Wilaya ya Mjini Unguja (10,722) lengo 19,272.

Mkuu wa Kurugenzi ya Huduma za Uchaguzi, Khamis Issa Khamis akizungumzia kuhusu uwekaji wazi orodha ya wapiga kura walioomba kuhamisha taarifa zao alisema, hadi kufikia juzi wapiga kura 302 wamewasilisha maombi.

Alisema uhamisho wa taarifa za wapiga kura ni endelevu na kazi ya kupokea taarifa za wanaoomba kuhamisha inaendelea kufanyika katika ofisi za uchaguzi za wilaya kila siku kwa saa za kazi.



Wanafunzi kutoka nchini Denmark, wakiwa Forodhani, mjini Zanzibar juzi, wakijiandaa kwa safari ya kwenda kisiwa kidogo cha Prison, kwa mafunzo na utalii. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Serikali yakiri kupanda kwa bei za bidhaa kutoka nje

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara, Maendeleo ya Viwanda Zanzibar imekiri kuwepo kwa upandaji wa bei za bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka nchi za nje.

Amesema hali hiyo inatokana na sababu tofauti zikiwemo za upungufu wa baadhi ya bidhaa katika masoko ya nje.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara, Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani katika kikao cha Baraza la Wawakilishi juzi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Jimbo la Paje, Dk. Soud Nahoda.

Mwakilishi huyo alihoji upandishaji wa bei ya vyakula na bidhaa kiholela akisema umekuwa ni tatizo kubwa visiwani hapa na kuongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wenye kipato cha chini, akihoji lini litatatuliwa tatizo hilo.

Akijibu swali hilo, Waziri Omar alisema sababu nyingine ni kupanda kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa kwa baadhi ya nchi na gharama za kubadilishia fedha za kigeni na kusababisha kuadimika kwa bidhaa hizo nchini.

Omar alisema serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda pamoja na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara ina utaratibu wa kufanya mapitio ya bei elekezi za bidhaa kwa zile zinazodhibitiwa pale inapohitajika kufanya hivyo.

"Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara Namba 5 ya Mwaka 2018 Kifungu Namba 5 (c) na 61 kinatoa mamlaka ya kupanga na kusimamia bei elekezi kwa bidhaa zinazodhibitiwa na Serikali kila panapokuwa na mfumko wa bei usiokuwa na sababu kwenye soko"alisema.

Alisema Wizara ya Biashara huwa inatangaza bei hizo kila panapotokea mabadiliko ya bidhaa hizo na suala hilo litapungua iwapo uzalishaji wa bidhaa muhimu utaongezeka.



**BABA LEVO**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI FEBRUARI 17, 2024



# MUNGU ATAWAZIBA MIDOMO

MSANII wa Bongo Fleva, Whozu, amezidi kumkingia kifua mpenzi wake Wema Sepetu, kwamba ipo siku Mungu atamfungulia na kupata mtoto wake.

Whozu ambaye anasifika kwa kuonyesha mahaba mazito kwa Wema, kiasi ambacho kila wakati anaibua hisia kali kwa mashabiki wake.

Hivi karibuni, Whozu ameweka wazi kwamba anaamini kuna siku watu watafungwa midomo baada ya mpenzi wake huyo kubeba ujauzito wake na hapo ndipo wataamini kwamba Mungu yupo.

Amesema kila watu wakimuandama Wema kwa maneno yao, huwa anapata nguvu zaidi na hajali wala hasikilizi maneno yao, anachoamini ni kwamba Wema Sepetu atamzalia mtoto.

"Mimi wala sifuati uzungu na ninaamini ipo siku nitazaa na Wema. Imani yangu bado inaniambia Mwenyezi Mungu atatubariki tutapata mtoto. Kwa hiyo ninamwambia kila siku kwamba usihofu, hutakiwi kuwaza sana, hutakiwi kuwaza vibaya," amesema.

Kauli hiyo ya Whozu, inatokana na baadhi ya watu kumuandama Wema kwa kutopata mtoto wakati umri wake unazidi kusonga mbele.

"Ninachoamini mimi na Wema tutaishi pamoja mpaka tupate mtoto mwingine ambaye atakuwa mdogo wake Lola," ameongeza

Whozu ameeleza kwamba wakiwa wawili wakati fulani wanakuwa na mawazo yanayosigana, ikiwa yeye anataka akipata mtoto awe wa kike, lakini Wema anapenda wa kiume.

**BASI SAWA**

## Nandy sasa hiyo sifa



SASA imekuwa kama sifa! Ndivyo anavyofanya msanii maarufu wa Bongo Fleva, Nandy, kutokana na nyimbo yake mpya 'Dah' kuendelea kushika namba moja katika majukwaa ya muziki.

Kama vile haitoshi, Nandy amejigamba kwamba pamoja na wimbo huo kuwa namba moja na remix yake imekamilika na wakati wowote ataitambulisha.

@Milioni 5 iko njiani, jamani dah! remix iko njiani na siku ya jumapili rasmi nitaitambulisha..!,@ ameandika mwanamuziki huyo kupitia ukurasa wake wa Instagram

Hivi karibuni, Nandy alifichua jinsi mwanamuziki wa Marekani Usher Raymond alivyopagawa na kibao hicho na kuomba apewe nafasi ya kuurudia tena.

## Mmelisikia tangazo la Uwoya?



MWIGIZAJI nyota wa Bongo Muvi, Irene Uwoya, amesema watu wengi wanaibiwa pesa zao na wajanja wa mjini ambao wanatumia jina lake vibaya.

Katika video aliyoiweka katika ukurasa wake wa Instagram, Uwoya amesema amekuwa akisema kila mara kwamba yeye hatoi mikopo wala misaada ya kifedha, lakini kuna watu wengi wanamsumbua baada ya kutapeliwa na watu hao.

"Kila mara natoa maelezo kwamba sitoi mikopo, lakini nashangaa watu wengi wanaendelea kutapeliwa na kuanza nisumbua. Nasisitiza sitoi mikopo wala hela kwa mtu yeyote," amesema Uwoya.



# BABA LEVO AKERWA VITUKO MAMA WENYE NYUMBA

MSANII wa muziki wa Bongo fleva, Baba levo, amekumbuka maisha yake ya kupanga nyumba za uswahilini, akisema kuna mama wenye nyumba wakorofi hawalipi bili za umeme.

Amesema wenye nyumba wengi hasa wanawake wanapangisha nyumba zao kwa mitego huku baadhi ya malipo kama umeme na maji wanaachiwa wapangaji pekee.

"Mimi nilikorofishana na mama mwenye nyumba baada ya kukataa kulipa bili ya maji na kutuachia sisi wapangaji. Nawaomba vijana wanaotaka kupanga wawe makini katika mikataba kwani kuna vipengele vinavyomlazimisha kulipia kila kitu," amesema.



# Vanillah ampa tano bosi wake

#MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi kutoka lebo ya Kings Music, Vanillah, amesema bosi wake Ali Kiba ana kawaida ya kuwashirikisha wasanii wake pale anapoandika wimbo mpya.

Amesema anamshukuru Kiba kwa kumkomaza kutokana na tabia yake hiyo kiasi ambacho anajivunia kila wakati kuwa kwenye mikono yake.

"Hakuna aliyemshawishi kunichukua kwenye lebo yake, namshukuru kwa kuona kipaji changu na sasa nipo kwenye timu yake na anaendelea kunishika mikono,@ amesema Vanillah.

# MIAKA MI 3 BILA SAUTI YA SONYO

**Na Adam Fungmwango**

IJUMAA ijayo Februari 23, mashabiki wa muziki wa dansi wataadhimisha miaka mitatu tangu kumpoteza mwanamuziki mwimbaji mwenye sauti nyororo, Waziri Sonyo.

Mwanamuziki huyo alifariki, 2021, usiku wa Februari 23 kwa ugonjwa wa moyo, muda mfupi tu baada ya kurejea kutoka kuangalia mechi ya mpira wa miguu, Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Simba dhidi ya Al Ahly ya Misri, ambapo Simba ilishinda bao 1-0, la Luis Miquissone.

Mwanamuziki huyo aliyezipigia bendi ya, Mviko Sound, Chuchu Sound, TOT Plus, African Revolution 'Tamtam', Double M na nyingine nyingi.

Amefariki Kibaha mkoani Pwani na kuzikwa huko huko akiwa na miaka 44

Zifuatazo ni nyimbo kali ambazo Sonyo aliziimba akiwa na bendi mbalimbali na kumpatia sifa kubwa.

### Usione Vyaelea-Chuchu Sound

Akiwa kwenye bendi ya Chuchu Sound, mwanamuziki huyo aliimba nyimbo mbalimbali ikiwemo 'Usione Vyaelea'.

Kwenye wimbo huo kuna sauti yake akiimba 'Kila ukionacho wataka kiwe chako, kila usikiacho wataka kukiona kwa macho.'

Ni moja kati ya nyimbo zilizoanza kuwafanya mashabiki wa muziki kuanza kumfuatilia na kukishangaa kipaji hicho kipya cha muziki, mwanzoni mwa miaka ya 2000.

### Masimango-TOT Plus

Huu ni wimbo wake maarufu zaidi kuliko zote alizowahi kutunga na kuimba. 'Masingango' ni wimbo uliotokea kupendwa na kuwa tishio akiwa TOT Plus na hapo ndipo kila mmoja akamjua Sonyo.

"Kwa kuwa vimekuwa dhahiri machoni mwangu, maji ya shingo yamenifika nashindwa kuvumia, ni bora kwetu kule alikobaki kaka..." Ni moja kati ya maneno aliyoyaimba kwenye wimbo huo bora kabisa.

### Sweet Baby-TOT Plus

Ni moja ya nyimbo safi ambazo ziliimbwa kwenye mtindo wa mduara hivi. Kipo kipande cha Sonyo ambacho aliimba 'Tulikuwa sote tulipata tabu, hatukujali maneno ya watu.'

Ni moja kati ya nyimbo zilizozidi kumpaisha Sonyo. 'Ilove Sweet Baby, nakupenda kwa dhati Sweet Baby, tumevumilia mengi Sweet Baba, sasa tuko fresh tunavinjari.' Hicho ni kiitikio cha ngoma hiyo.

### Mengi Yamenikuta-Tamtam

Akiwa na African Revolution waka 'tamtam', Sonyo alitunga na kuimba kibao kimoja kiitwacho 'Mengi Yamenikuta.'

Katika wimbo huo anasema yaliyomkuta ndiyo ya kidunia, kwani hata Yesu, pamoja na mafundisho yake mazuri, lakini Wayahudi walimkatana, kumpiga na kumtesa, sembuse yeye hatoshangaa.

### Ndoto-Jiti



Wimbo huu ulipigwa kwenye mahadhi ya muziki wa kisasa. Alishirikishwa na msanii aitwaye Jiti.

Ni msanii aliyekuwa akiimba nyimbo za Hip Hop, hivyo akamshirikisha Sonyo ili kuweka ladha ya sauti yake nyembamba na kuimba, ili mashabiki wapate ladha mbili kwa wakati mmoja, kufokafoka na kuimba.

**FILAMU**

# Mapenzi yamekufa, yameoza

**Na Adam Fungamwango**

"JUNAH, mapenzi kwangu yalishakufa."

"Mimi nina imani kuwa wewe ni mwanaume sahihi, nakupenda Ismail. Unaweza ukawa baba wa familia yangu!"

"Junah wewe ni mgeni maeneo haya, hayo mapenzi unayozungumza wewe, ndiyo yaliyonifanya mimi nimepoteza hata macho yangu. Na hata aliyesababisha haya yote hayupo tena kwenye nuru ya macho yangu."

Ni mazungumzo kati ya kijana mlemavu wa macho Ismail na msichana Junah. Mwanamke anaonekana kumzimia mwanaume, lakini mwenyewe hataki hata kusikia hayo mapenzi.

Kisa hiki kipo kwenye filamu kali iitwayo, 'Mapenzi Yamekufa.' Ni filamu ambayo inaweza kukutoa machozi, lakini pia kukupa ujumbe amabo utaishi nao siku zote.

Imetungwa na Ismail Ramadhani na mwenyewe akacheza kama Ismail, huku wengine walioshiriki ni Ramadhani Athumani aliyecheza kama Yusuph, Hawa Abel akicheza kama Junah, Mariam Bahati yeye aliekti kama Halima, Christina Julius.

Siyo kawaida kwa binadamu kukataa kupendwa. Tatizo ni nini? Kuna kitu kilitokea miaka mingi nyuma.

Alikuwa na mke aliyeitwa Nina. Alikuwa na macho yake kama watu wengine. Awali aliishi vyema na mkewe, lakini akapata shoga ambaye alimbadilisha tabia.

Akawa anamuuza kwa wanaume wengine. Mume akagundua. Mke akatoa na ujazito wa Ismail kwa sababu tu apate nafasi ya kustarehe na mabwana wengine.

Siku isiyo na jina alimbamba laivu mkewe akiwa ameingiza mwanaume ndani. Wakati Ismail anamuadhibu jamaa, mkewe akaenda kuchukua kitu kizito na kumpiga nacho kichwani, ambacho kilimsababishia ulemavu wa macho.

Tangu hapo kwake mapenzi yakawa yamekufa. Junah, binti mrembo alijitokeza kumpenda Ismail. Akawa anamletea chakula kila siku nyumbani kwake. Akashawishi awe mpenzi wake, ikiwezekana amuoe. Ismail alikataa. Akajua baadaye yatakuwa ni yale yale tu.

Ilimuumiza mno Junah. Kuna siku alimkuta akiwa amekaa na msichana Halima. Moyo ukawaka. Akalia kwa kwikwi. Huruma ikamjia Ismail. Akamwambia Junah, Halima si mpenzi wake, ila ni rafiki yake kwani huwa anasuluhisha ugomvi wake na mpenzi wake. Ni siku ambayo Ismail alikubali ombi la Junah. Kweli alitambua kuwa anampenda. Wakakumbatiana.



BT BURUDANI TELE




# Timini watakuelewa tu

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Timini amesema wanaume wanaweza kupata uzoefu wa kupata mchumba kutoka kwa wanawake wa Nigeria wanaoishi nje ya nchi hiyo.

"Kwa kweli ninahisi kutokana na uzoefu wangu binafsi, ninahisi utapata uzoefu mzuri wa kupata mchumba kutoka kwa msichana wa Kinigeria wanaoishi ng'ambo wanayeishi hapa nchini," amesema.

Muigizaji huyo amesema kuwa wanawake wanaoishi Nigeria wanachagua wanaume, lakini wenzao walio ng'ambo hutumia tovuti kutafuta wapenzi kwa sababu ya kuwa wachache.



## Portable suluhu sio kuacha mke

MWANAMUZIKI maarufu katika mitaa ya uswahilini nchini Nigeria, Portable amesema endapo atagundua wake zake wanatoka na wanaume wengine, atawaacha kwa sababu hataki kufa akiwa bado kijana.

Mwimbaji huyo alitoa msimamo huo kupitia ukurasa wake wa Instagram, na kuwataka wanaume wengine kuchukua hatua hiyo kwani suala hilo halina mazungumzo.

"Ikiwa kuna yeyote kati ya wake zangu atanidanganya na mimi nitawaacha kwa sababu sitaki kufa kijana. Ikiwa mke wako anakudanganya na wewe hufai kuzungumza naye, hiyo ina maana wewe si mwanaume wa kuwajibika,"ameandika.

## Burna Boy kumbe mtata

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria, Burna Boy amezidisha taharuki baada ya kuongeza moto katika ugomvi wake na msanii mwenzake, Davido, kwa kumtusi hadharani.

Burna Boy ametumia mtandao wa X kutoa kauli hiyo baada ya mtumiaji mmoja kumtaka kuondoa tofauti zao hasa kwa kuzingatia Davido ndiye aliyemtoa kimuziki.

Mwanamuziki huyo wa AfroBeats, alikasirishwa kwa kitendo cha mtu huyo kumtaka atoe sababu za kumchukia Davido, na kumuita Burna Boy kama mtu mwenye kiburi na asiye na shukrani.





## Nani kasema Usher hapati jiko?

MKALI wa muziki wa R&B kutoka Marekani, Usher Raymond amefunga ndoa na mpenzi wake wa muda mrefu, Jennifer Goicoechea.

Harusi hiyo iliyofanyika Februari 11 huko Las Vegas ilishuhudiwa na mama yake, Jonetta Patton, ilikuwa ya kifahari na kuhudhuriwa na marafiki na familia ya wanandoa hao.

Msemaji wa Usher alithibitisha kuwepo kwa tukio hilo na kueleza furaha ya wanandoa hao kuanza safari mpya kama mume na mke.

## Mo'Nigue unamchokoza shetani aliyelala

MWIGIZAJI na mchekeshaji maarufu wa Marekani, Mo'Nique ameendeleza ugomvi wake na mtangazaji mkongwe Oprah Winfrey akimuelezea kama mwanamke anayejivuna.

Mo'Nique, ambaye alikuwa akizungumzia changamoto zake za uigizaji huko Hollywood, amesema yeye na Winfrey wana pengo kubwa la malipo ambalo linawaathiri wanawake weusi katika tasnia ya burudani.

"Ona, ninapozungumza kuhusu Oprah Winfrey na niseme wazi kuwa ninampenda dada huyu mbinafsi, lakini mwanamke huyo ananisema vibaya kuhusu mimi. Kimsingi hakuna usawa Hollywood kuna changamoto nyingi zinazowakabili wasanii weusi katika malipo,"amesema.



## WWF yapata mwarobaini tembo kuvamia makazi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SHIRIKA la Wanyamapori Duniani (WWF) limewezesha ujenzi wa mabwawa ya maji kwa ajili ya wanyamapori na kukabiliana na changamoto ya kuvamia makazi ya watu.

Hayo yalisemwa mjini hapa Mkoa wa Kilimanjaro na Mtaalam wa Wanyamapori wa WWF, Noah Sitati wakati wa warsha ya mafunzo ya Ufuatiliaji wa Taarifa za Maeneo (SMART) kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu za maliasili katika maeneo ya uhifadhi na jamii.

Sitati, alisema ili wanyamapori waweze kustawi, maji ni muhimu, hivyo WWF ikaja na wazo la mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya wanyama hao ili kupunguza hatari kwa kuingia katika makazi ya watu na kuharibu miundombinu ya maji na mazao mashambani.

"Mabwawa haya yamejengwa katika maeneo ambayo yana historia ya mvua chache na ukame, mambo ambayo yanaathiri kwa kiasi kikubwa idadi ya wanyamapori, maeneo hayo yapo Same, Mwanga, Rombo, kwa kutaja machache tu," alisema.

Akizungumzia kuhusu mafunzo hayo, Sitati alisema yamelenga kutoa elimu kwa wasimamizi wa wanyamapori jinsi ya kukusanya takwimu sahihi kwa kutumia teknolojia ya kisasa zitakazowezesha mamlaka husika kukabiliana na changamoto kuhusu wanyamapori.

Mtaalamu wa Tembo na Faru wa Wilaya ya Same, Kolady Kayanda,alisema mafunzo hayo yatawawezesha wasimamizi wa wanyama hao kupata na kuhifadhi taarifa za maliasili vizuri.

"Zamani walikuwa wakitumia vitendea kazi duni kwa mfano madaftari hali ambayo wakati mwingine ilipelekea kupoteza taarifa muhimu kuhusiana na maliasili ambazo zinahitajika ili kukabiliana na changamoto kuhusu uvamizi wa wanyamapori," alisema na kusisitiza kuwa:

"Mafunzo haya yatawajengea uwezo wataalamu wa usimamizi wa wanyamapori katika vijiji na kata kutumia teknolojia ya kisasa kukusanya taarifa na kuziwasilisha mamlaka husika kwa wakati, hii itatoa mwanga kwa mamlaka husika kukabiliana na changamoto hizo kwa haraka." .

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Same, Thomas Katunzi alilishukuru WWF kwa kufanikisha mafunzo hayo na shughuli nyingine kuhusiana na uhifadhi wa wanyamapori na maliasili kwa ujumla.

Akizungumzia mafunzo hayo, Katunzi alisema yataleta mapinduzi makubwa katika uhifadhi wa taarifa kuhusiana na maliasili na wakazi wanaoishi maeneo ambayo yameathiriwa na uvamizi wa wanyamapori hasa tembo.

# Kata za Simanjiro zazingirwa na mafuriko

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wameiomba Serikali kuwanusuru na maafa wakazi wanaoishi kata zilizozingirwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua.

Wametoa ombi hilo baada ya mvua kubwa kunyesha juzi na kusababisha baadhi ya nyumba za vijiji vya kata za Shambarai na Ngorika kuzingirwa na mafuriko hayo, miundombinu ya barabara kuharibika na mawasiliano kukatika.

Diwani wa Ngorika, Albert Msole akizungumza juzi, alisema baada ya mvua hizo kunyesha bwawa la Nyumba ya Mungu limefurika, mawasiliano eneo linalounganisha Kijiji cha Nyumba ya Mungu na mengine ya Kata ya Ngorika na Wilaya ya Simanjiro yamekatika.

Msole, alisema eneo hilo ni hatari kwa maisha ya watu wanaotumia mitumbwi kuvuka kwenda kwenye shughuli zao na kwa wanafunzi wanaoishi Kijiji cha Nyumba ya Mungu shuleni.

"Ni hatari zaidi kwa wagonjwa hasa kina mama wanaokwenda kupata huduma za matibabu na kliniki, tunaomba tupate kivuko ili kurahisisha huduma kwa wananchi wanaoishi kuzunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu," alisema Msole.

Alisema miundombinu ya mawasiliano nayo inapaswa kurejeshwa kati ya Kijiji cha Nyumba ya Mungu na Kata za Ngorika na Kijiji cha Ngage Kata ya Loiborsoit na Wilaya ya Simanjiro baada ya kuharibiwa na mvua hizo.

Diwani wa Kata ya Shambarai, Julius Mamasita, alisema mafuriko hayo yameharibu baadhi ya nyumba na mashamba ya wakazi wa eneo lake.

"Tunaiomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma kwani ukitaka kwenda hata mji mdogo wa Mirerani inakupasa upitie wilaya jirani ya Arumeru mkoani Arusha kutokana na eneo letu kukumbwa na mafuriko," alisema Mamasita.

Diwani wa Kata ya Loiborsoit, Siria Baraka Kiduya, alisema wakazi wa Kijiji cha Ngage wanashindwa kwenda kata jirani ya Ngorika hasa Kijiji cha Nyumba ya Mungu kutokana na mafuriko hayo.

"Tunaomba Serikali iingilie kati kwa kuhakikisha miundombinu ya barabara inatengenezwa baada ya kuharibiwa na mafuriko," alisema Kiduya.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher ole Sendeka, alisema ametembelea maeneo hayo na kushuhudia changamoto hiyo.

"Tunaomba itusaidie kwani mafuriko haya yametuathiri mno na kusababisha shughuli za maendeleo kukwama," alisema Sendeka.

Alisema hivi karibuni uongozi wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) ulitembelea eneo la Msitu wa Tembo na kushuhudia miundombinu ya barabara ilivyoathiriwa na mvua hizo.



Mbunge wa Moshi Mjini, mkoani Kilimanjaro, Priscus Tarimo, akizungumza na wafanyabishara wadogo wa Soko la Mbuyuni, lililoteketea kwa moto hivi karibuni, alipofanya ziara mapema wiki hii, kwa ajili ya kuwapa pole waathirika na kuangalia maendeleo ya kurudisha hali ya soko hilo. **PICHA: JAMES LANKA**

# Moto wazua taharuki NSSF, wajeruhi

**Na Oscar Assenga,** TANGA

TAHARUKI imewakumba wateja na wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) mkoani hapa kutokana na kila mmoja kutaka kuokoa maisha yake baada ya moto kuzuka ndani ya chumba kilichopo kwenye jengo la ofisi hizo.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapa, Mrakibu Abrhaman Ntezidyo alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi majira ya saa 4:40 asubuhi.

Ndezidyo, alisema walipataa taarifa kutoka kwa Meneja wa NSSF mkoani hapa, Nuhu Mmbaga kuwa moto huo unawaka kwenye chumba hicho na kuwahi kwa ajili kuuzima.

Alisema kwenye chumba hicho kulikuwa na vitu kadhaa, ikiwemo thamani za ofisi na kwamba walidhibiti moto huo kwa kuuzima kabla ya kusababisha madhara makubwa.

Alisema walikuta taharuki ambazo zilisababisha mmoja wa wafanyakazi hao kujeruhi kwa kupata mshtuko na kupelekwa hospitalini kwa matibabu.

Hata hivyo, alisema chanzo cha moto huyo hakijafahamika, wanaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini na kutoa taarifa baada ya kukamilika.

Alitoa wito kwa wananchi wanapopata matukio ya moto kutoa taarifa mapema ili jeshi hilo lifike mapema kudhibiti na kuokoa mali na watu.

Awali Meneja Mmbaga, alilishukuru jeshi hilo kwa kuwahi kufika kwenye eneo la tukio na kudhibiti moto huo.

# Polisi kata waagizwa kutenda haki

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi wilayani hapa Mkoa wa Tanga limewaagiza wakaguzi wake wa kata kufanya kazi kwa uadilifu na kutenda haki kwa wananchi na watumishi. Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Wilaya hiyo, Charles Ntenga kwa wakaguzi hao wa zaidi ya kata 20 katika hafla ya kufahamiana na kubadilishana uzoefu wa utekelezaji wa majukumu yao.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) hiyo, Hadija Sokolo, alisema wakaguzi hao wanatakiwa kuongeza bidii katika utoaji elimu kwa wananchi kwenye kata zao ili kupambana na kudhibiti uhalifu.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani hapa, Leonard Bandola, aliwapongeza wakaguzi hao wa polisi kata kwa kupeana uzoefu kuwa utawasidia katika majukumu yao.


Mkaguzi wa Polisi Kata ya Magila, Frank Mwemsi, aliahidi wataongeza bidii katika utoaji elimu kwa wananchi kwenye kata zao ili kupambana na kuzuia uhalifu kupitia ulinzi shirikishi kwa kuwa ni mwarobaini wa vitendo hivyo nchini.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Mbongo aliyeimba wimbo 'Malaika' ukatajirisha wengine, akafa masikini

## -Alimwimbia mpenzi wake kwa kukataliwa na wazazi

**Na Adam Fungamwango**



Makeba



Malaika

MALAIKA, nakupenda Malaika, nami nifanyeje, kijana mwenzio. nashindwa na mali sina weee, ningekuoa Malaika. Kidege, hukuwaza kidege. Ningekuoa aaa mama, ningekuoa aaa dada, nashindwa na mali sina wee, ningekuoa Malaika. Pesa zasumbua roho yangu, nami nifanyeje, kijana mwenzio, nashindwa na mali sina wee, ningekuoa Malaika."

Ni zaidi ya miaka 70 sasa tangu utungwe na kurekodiwa, lakini hadi leo umekuwa moja ya nyimbo bora kabisa duniani zinazoendelea kuishi na kuzidi kupendwa kizazi hadi kizazi kinachofuata.

Huwezi kwenda kwenye bendi yoyote ile inayopiga laivu, duniani, bila ya wimbo huo kupigwa, kwa kuimbwa au vyombo vitupu. Kwa sababu umekuwa wimbo mkubwa mno duniani, kuna utata mkubwa kuhusu mtunzi halisi wa wimbo huo.

Waandishi, wafuatiliaji wa masuala ya muziki na watafiti, walifanya uchunguzi huku na huko kujua ni nani hasa mtunzi halisi wa wimbo huo.

Awali kabisa ni wimbo ambao umerekodiwa na bendi nyingi sana duniani kuanzia kundi maarufu la Boney M lililovuma sana miaka ya 1970, lenye makazi yake nchini Ujerumani, Miriam Makeba na Harry Belafonte, Angelique Kidjo, Pete Seeger na wanamuziki wengi sana duniani, waliurekodi wimbo huu wakiimba kwa lugha hiyo hiyo ya kiswahili.

Pamoja na kutumia lugha ya kiswahili, kila mmoja kwa staili yake, na mtindo wake wa muziki walioamua kupiga.

Mtu aliyenufaika sana na wimbo huu, kwa kulipwa mirahaba na makundi yote yaliyotaka kupiga kuonana naye na kumlipa kwanza ni Fadhili William. Huyu ni mwanamuziki maarufu sana wa Kenya aliyezaliwa mwaka 1938 na kufariki Februari 11 mwaka 2001.

Ingawa alitunga, kupiga na kurekodi nyimbo nyingi kama 'Taxi Driver', 'Ewe Wangu', 'Naenda Safari' na zingine nyingi, lakini wimbo uliomfaidisha na kumpa maisha mazuri ni 'Malaika' aliourekodi mwaka 1963 na bendi yake ya Jambo Boys. Yeye ndiye aliyeusajili kama mtunzi halisi, na aliyekuwa na hakimiliki ya wimbo huo.

Ni wimbo uliompa pesa nyingi sana kwa bendi nyingi kutaka kurekodi, hadi alipofariki dunia.

Hata hivyo wale wachunguzi wa masuala ya muziki wakaja kugundua utata mwingine.

Wakatajwa watunzi wengine kuwa ni Lucas Tututu wa Mombasa, lakini pia Andrea Sholo naye akatajwa kuwa mtunzi.

Baadaye, ikaja kugundulika kuwa mtunzi halisi ni mtu mmoja Mtanzania, anayeitwa Adam Salim.

Wachunguzi wengi, waandishi wa habari na wadau wa muziki, mwisho wao walifikia hapo na wakakubaliana hivyo.

Mtanzania huyu mwenyeji wa Moshi mkoani Kilimanjaro aliyezaliwa mwaka 1926, ndiye aliyeutunga wimbo huo. Ndiye mtunzi halisi wa wimbo 'Malaika', lakini hakupata chochote zaidi ya shilingi 60 alizolipwa alipokwenda kuurekodi na kuuza kwenye kampuni ya kurekodia Columbia East African Music Company mwaka 1950.

Ingawa kwa wakati huo zilikuwa nyingi, lakini hapo ilikuwa ndiyo mwisho wa kupata pesa zingine, kwani baadaye ilikuwa ni kama ameuza hakimiliki. Sijui nini kilitokea, wimbo huo baadaye ukaja kuchukuliwa na Fadhili William kuwa ndiye mtunzi na aliyefaidika kwa mirahaba kutoka pande zote za dunia.

Kuna baadhi waandishi wa habari za uchunguzi walidai, mtunzi huyo alipata habari za msiba na mama yake, akalazimika kurejea Moshi, lakini hakurejea tena Kenya, hivyo hakimiliki ikachukuliwa na Fadhili ambaye ndiye alikuwa mtu wa karibu na inadaiwa kuwa ndiye aliyempa nauli na pesa zingine za kwenda kufanya mazishi nyumbani kwao.

Dhana nyingine kutoka kwa waandishi inadai kuwa Adam alipata ajali akafariki dunia alipokuwa akirejea nchini Kenya baada ya mazishi ya mama yake.

Ukweli unabaki pale pale kuwa aliporejea kwao Moshi, hakurejea tena nchini Kenya hadi leo hii na Moshi hakuonekana tena.

Waandishi wakagundua kuwa wimbo huo, Adam alimtungia mpenzi wake aliyeitwa Halima Ramadhani Maruwa aliyekuwa akiishi Kenya.

Mbongo huyo akiwa nchini Kenya, alikuwa akifanya kazi ya umakenika, au siku hizi wanaita fundi gereji, lakini pia ni mwanamuziki aliyekuwa na bendi yake akiita Adam & Trio iliyokuwa ikipiga muziki kila wiki kwenye mahoteli na baa mbalimbali.

Akampata mrembo huyo ambaye walipendana sana.

Hata hivyo wazazi wa Halima hawakumpenda Adam, licha ya binti mwenyewe kulalamika sana, lakini haikusaidia. Kuwa mwanamuziki pia kulichangia sana wazazi hao kukataa binti yao asiolewe naye.

Kwanza wazazi msichana huyo walikuwa itikadi na imani yao haikuendana na muziki, halafu mara nyingi kuna dhana kuwa wanamuziki ni watu wasiotulia, wahuni, hivyo binti yao anaweza kutopata matunzo mazuri, akateseka.

Kisa hiki kilimalizika kwa binti huyo kuolewa na mwanaume mmoja tajiri mwenye asili ya kiasia.

Hilo lilimuumiza sana Mtanzania huyo, ndipo akautunga wimbo huo kama unavyojieleza, kuwa anampenda sana, lakini afanye nini, mali hana, kama angekuwa na pesa angemuoa malaika huyo.

Watu wa karibu na Adam wanasema alianza kwa kuandika barua. Alimuandikia barua ya huzuni mpenzi wake Halima, na baadhi ya maneno yaliyokuwa kwenye barua hiyo, ndiyo aliyachukua baadaye na kuyafanya mashairi ya wimbo huo.

Kwa uchache hicho ndicho kisa cha wimbo wa 'Malaika' uliotungwa na Mtanzania Adam na kumnufaisha Mkenya Fadhili.

Mtanzania huyo alitunga kwa huzuni ya kunyimwa mpenzi wake aliyeolewa na tajiri. Alifanya hivyo ili tu kutoa la moyoni mwake badala ya kukaa nalo rohoni. Akaufanya wimbo, akaurekodi, bila kujua kuwa utakuwa wimbo mkubwa sana duniani utakaotengeneza mamilioni ya pesa ambayo hakubahatika kuyapata. Bahati mbaya sana kama alivyokataliwa na wazazi wa binti na kutoishi naye kwa muda mrefu, pia hakunufaika sana na wimbo wa 'Malaika.'

**Tuma meseji 0716 350534**



Boney-M

HABARI KIMATAIFA

# Kiongozi upinzani Russia afariki gerezani

**MOSCOW, Russia**

KIONGOZI mkuu wa upinzani nchini Russia, Alexei Navalny, amefariki dunia jana akiwa gerezani.

Taarifa kutoka mashirika ya habari nchini humo yalinukuu tangazo la kifo cha Navalny kutoka jeshi la magereza la nchi hiyo.

Navalny ambaye amekuwa mkosoaji mkubwa dhidi ya Rais Vladimir Putin, alikuwa akitumikia kifungo cha miaka 19 jela kwa makosa yanayochukuliwa kuwa yanachochewa kisiasa.

Mwishoni mwa mwaka jana, alihamishwa gereza la Arctic, ambalo linaaminika kuwa moja ya jela zenye ulinzi mkali zaidi.

Kulingana na shirika la habari la Tass, idara ya magereza katika wilaya ya Yamalo-Nenets ilitoa sababu za kifo chake.

Gereza hilo lilieleza kwamba Navalny alijisikia vibaya baada ya matembezi siku ya Ijumaa.

"Alipoteza fahamu, timu ya matibabu ya dharura iliitwa mara moja na kujaribu kumzindua lakini bila mafanikio ilisema taarifa hiyo.

Hata hivyo wakili wake, Leonid Solovyov, alisema madaktari wa dharura walitangaza kuwa mfungwa huyo amekufa lakini hawakutoa sababu ya kifo chake.

Shirika la habari la Interfax, lilidai kuwa gari la kubebea wagonjwa lilifika kwenye gereza hilo ndani ya dakika saba, huku madaktari wakitumia nusu saa kujaribu kumzindua Navalny.

"Muda wa kupeleka gari la wagonjwa ulikuwa chini ya dakika saba. Madaktari walifika eneo la gereza kumwona mgonjwa dakika mbili, waliofika eneo la tukio waliendelea na hatua za kumzindua ambazo tayari zilikuwa zimetolewa na madaktari wa gereza.Walitumia zaidi ya nusu saa. Hata hivyo, mgonjwa alifariki," Ilisema taarifa ya Hospitali ya Jiji la Labytnang.

# Israel isishambulie mji wa Rafah

**WASHINGTON, Marekani**

SERIKALI ya Israel inaendelea kupata shinikizo kali kutoka kwa mshirika wake mkuu Marekani dhidi ya uamuzi wake wa kufanya mashambulizi katika mji wa Rafah ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Mji huo una zaidi ya Wapalestina milioni 1.5 wamekimbilia kujihifadhi kutokana na mashambulizi ya Israel yanayoendelea katika maeneo mengine.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu ameapa kuendelea na kile alichokiita oparesheni kubwa katika mji huo ili kupata ushindi kamili dhidi ya kundi la Hamas.

Ikulu ya Marekani ilisema jana kuwa Rais Joe Biden amefanya mazungumzo kwa njia ya simu na Netanyahu jana jioni, na kumhimiza kutofanya shambulio katika mji huo.

Licha ya wito huo, waziri mkuu huyo alisisitiza Israel haitakubali maagizo ya kimataifa katika mzozo kati ya nchi yake na kundi la Hamas.

Hadi sasa maelfu ya watu wamekimbia makazi yao katika ukanda wa Gaza na kuelekea mjini Rafah wakitafuta hifadhi katika kambi za muda zilizoenea karibu na mpaka wa nchi ya Misri.

Kulingana na shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu misaada ya kibinadamu OCHA, mji huo umehifadhi zaidi ya nusu ya wakazi wa Gaza, huku watu hao wakirundikana katika eneo moja.

Nchi za Uingereza, Australia, Canada na New Zealand pia zimetoa wito kwa Israel kutofanya mashambulizi ya ardhini katika mji huo wa Rafah.

Ofisi ya Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak, ilieleza kuwa kiongozi huyo alifanya mazungumzo kwa njia ya simu na Netanyahu akielezea wasiwasi wa nchi hiyo kuhusu jinsi hali ilivyo katika mji huo na hali mbaya ya kibinadamu inayoweza kutokea iwapo Israel itaendelea na oparesheni yake ya kijeshi.00:56

Wakati huo huo, Israel imeripoti kifo cha mwanajeshi wake mmoja katika mapigano yanayoendelea ukanda wa Gaza jana.

Iliongeza kwamba idadi ya askari wake waliouawa tangu ilipoanzisha mapigano ya ardhini dhidi ya Hamas kufikia 233.

Hata hivyo, wapatanishi kutoka mataifa ya Marekani, Qatar na Misri wamekutana mjini Cairo ili kusaka makubaliano mapya ya kusitisha mapigano na kuhakikisha watu walioshikiliwa mateka na Hamas wanaachiliwa kwa mabadilishano na wafungwa wa Kipalestina.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken alisema anaamini makubaliano ya kusitisha mapigano yanawezekana kuafikiwa siku chache zijazo.

"Tunaamini lazima suala la kuachiliwa huru mateka lipewe kipaumbele, na kuwarudisha nyumbani kwa wapendwa wao," alisema Blinken.

Mkurugenzi wa shirika la kijasusi la Marekani la CIA, Bill Burns, juzi alifanya ziara ya siri nchini Israel kwa ajili ya mazungumzo na Netanyahu na mkuu wa shirika la kijasusi la Israel la Mossad, David Barnea.

**DW**



Watoto wa Kipalestina wakikagua nyumba iliyoshambuliwa na jeshi la Israel katika mji wa Rafah jana.**PICHA: REUTER**

# Mahakama Senegal yatengua amri ya kuahirisha uchaguzi

**DAKAR, Senegal**

MAHAKAMA ya juu nchini Senegal imebatilisha agizo la Rais Macky Sall la kuahirisha uchaguzi mkuu na kueleza hatua hiyo ni kinyume na katiba ya nchi hiyo.

Aidha, mahakama hiyo pia imekataa muswada tata uliopitishwa na bunge kusogeza mbele tarehe ya uchaguzi huo ambao ulipangwa kufanyika mwezi huu.

Maandamano makubwa yameikumba nchi hiyo ya Afrika Magharibi, ambayo wakati mmoja ilichukuliwa kama taifa lenye demokrasia katika eneo hilo.

Kambi ya upinzani iliyoandaa maandamano hayo ilisema kuahirishwa kwa uchaguzi ni sawa na mapinduzi ya kitaasisi.

Rais Sall alikuwa ametangaza kuahirisha uchaguzi huo kwa sababu ya kile alichodai kuwa ni wasiwasi kuhusu wagombea wa upinzani kukosa haki.

Pendekezo lake lilikuwa limeungwa mkono na wabunge 105 kati ya 165.

Hapo awali ilipendekezwa uchaguzi huo ungefanyika baada ya miezi sita, lakini marekebisho ya dakika za mwisho yalizidisha muda huo hadi Desemba 15, sawa na miezi 10.

Awali, Rais Sall alikaririwa akieleza hakuwa na mpango wa kuwania wadhifa huo tena. Lakini wakosoaji wake walimshutumu kuwa anajaribu kung'ang'ania madarakani kwa njia ya nyuma. Kutokana na hukumu hiyo, wagombea wa upinzani na wabunge ambao walikuwa wamewasilisha pingamizi kadhaa za kisheria dhidi ya muswada huo, walifurahishwa na hukumu hiyo.

Khalifa Sall, mpinzani mkuu na meya wa zamani wa mji mkuu wa Dakar, ambaye hana ujamaa na kiongozi wa sasa, alitaja kucheleweshwa kwa uchaguzi kama mapinduzi ya kikatiba.

Mgombea mwingine, Thierno Alassane Sall, aliitaja hatua hiyo kama uhaini wa kutisha.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI GARI

**THADEUS CHARLES KESSY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI NAMBA T 755 APM AINA YA NISSAN J86 RANGI NYEUSI , ENGINE NAMBA ZD30051122K, CHASISI NAMBA ADNH860000E000621B, YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI **TAARIFA PHQ/DAR/UBU/18995/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI GARI

**NDUGU NESTORY ERASTO CHOYANGENEYE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA GARI AINA YA TOYOTA RAV 4 LENYE NAMBA ZA USAJILI T388 CCY ILIYOSAJILIWA KWA MAJINA YA HAWA MOSHEZI AMRI. AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA**PHQ/KAG/BUK/1393/2024.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI AU AWASILIANE NAYE KWA **NAMBA 0612666500.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...01/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MAZIKU SAID KAVERA wa MWEMBESONGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA KAVERA MAZIKU SAID**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 27 Mwezi 02 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo tarehe 29 mwezi 1 mwaka 2024**

## NOTES OF VALUNTARY WINDING UP THE COMPANY

**JOURNEYS 2 EXPEDITION TRAVEL AGENCY LIMITED**

***Certificate of incorporation number 156-623-997***

**The following resolution be adopted**

1. That we would like to give notice to the public that **JOURNEY 2 EXPEDITION TRAVEL AGENCY LIMITED,** the company with incorporation number 156-623-997 that due to operational difficulties members of the company decided to wind up the company voluntarily.

2. That, the notice is hereby given to all creditors stake holders and public at large that it there is any objection(s)or claim (s)should be directs to **MICHAEL ANDREW KIVARIA(COMPANY SECRETARY)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 33/2024**
**Jina la Mdai: TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE**
**Jina la Mdaiwa; MWAMINI MUDDY MUSTAPHA**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: MWAMINI MUDDY MUSTAPHA**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba

**UNATAKIWA KUFIKA KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI BILA YA KUKOSA SIKU HIYO MADAI YA PESA 1,628,100/-**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 27 Mwezi 02 Mwaka 2024 saa 08:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 14 Mwezi 02 Mwaka 2024.

HAKIMU

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.**
**TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**E-MAIL: advertise@guardian.co.tz**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu.

Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa.

Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba.

Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu.

Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

# Mama mwenye nyumba-15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Devota akarudia tena swali lile lile baada ya kuona hajibiwi. Safari hii akajibiwa.

"Siyo kweli, sijawahi kusema hivyo! Aliyekwambia ni mbea na mnafiki." Akajibu.

"Wewe, mimi nina ushahidi hadi sauti yako na video watu walikuwa wanakurekodi ulivyokuwa unaongopa."

Ni kweli. Watu walimrekodi Mwantumu.. Wengi walichoshwa na tabia yake ya ushakunaku, umbea na uzandiki. Kipande hicho wakamtumia mwenyewe.

Hakuwa mjinga kufunga safari kutoka Kinondoni hadi Magomeni kwa maneno matupu.

Akachukua simu yake na kubonyeza vitufe kadhaa ili kuifungua nywila, baadaye akafungua eneo la kuonyesha video na sauti.

Wakati huo tayari umati wa watu ulikuwa uameshajaa eneo hilo kama ilivyo kawaida tu ya uswazi. Watu wasisikie kitu.

Kitu kitu kilisikika. Hata vile ambavyo hakuambiwa. Mwantumu aliona aibu na watu waliokuwa hapo wakaanza kumcheka, kumzodoa.

"Haya sasa, wewe umesema nimewekwa bure, sasa ngoja nikuonyeshe mkataba wangu."

Akatoa makaratasi yake ya mkataba na kumuonyesha. Hata hivyo Mwantumu alikuwa haangalii. Macho yako yaliangalia chini kwa aibu.

"Soma sasa. Kuna sehemu imeandikwa mimi ni mlinzi wa ile nyumba? Hivi nikufanyeje wewe?"

Wakati huo baadhi ya akinamama waliochoshwa na tabia za Mwantumu wakaanza kumzomea na kuimba.

"Kokoriko umbea uache, kokoriko umbea uache..." Hasira zilimpanda Devota, akajikuta, akamkamata mkono na kumvuta mbele yake.

Mwantumu alivutika na kuja mbele yake. Kilichotokea ni kwamba Devota alimkamata kama wacheza mieleka na kumlalia chini.

Devota juu, Mwantumu chini, ndiyo hali ilivyokuwa. Devota alionekana kujiweza zaidi kwa sababu alijiandaa na tukio hilo kuliko mwenzake.

Khanga aliyokuwa amevaa Mwantumu nayo ilichangia kumweka kwenye hali ngumu kwani ilimzingira na kujifunga kichwani kiasi cha kumfanya asipumue vizuri.

Ukichangana na kwamba alikuwa chini ya mwenzake aliyekuwa akimshindia ngumi, ingawa zilikuwa dhaifu.

Kelele na akinamama na watoto ziliwashtua baadhi ya wanaume waliokuwa wanapita na shughuli zao, wengine wakiwa wamejipumzisha ndani.

Wakakimbilia eneo la tukio na kuta 'ndundi'. "Hivi nyingi mnashangilia huu upuuzi, watu wanaumizana nyingi mnaona raha!" Kijana mmoja jirani anayeitwa Juma alikuwa mmoja aliyefika pale na akaanza kazi ya kuwang'atua chini walipokuwa wakipigana.

Wanaume wengine wakamsaidia Juma na kufanikiwa kuwaachanisha.

"Ungeacha tu apigwe, kazidi umbea huyu mama." Ilikuwa ni sauti ya Tabia akimwambia Juma.

"We Tabia umehama wewe, umekuja kufanya nini tena?" Akauliza Juma na akajibiwa, "Nimeufuata kushuhudia huu huu ugomvi."

Yote yakiwa yanendelea, ghafla ugeni mkubwa ukawasili. Alikuwa ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mitaa, Mjumbe ya Nyumba Kumi na Polisi Jamii mmoja.

Ni wale wale waliofika kwenye tukio la fumanizi la Peter mume wa Devota na binti wa Mwantumu, Mwadawa.

Polisi Jamii akawaweka wote wawili chini ya ulinzi. "Nyinyi, ule ugomvi wenu wa fumanizi bado haujaisha tu?" Akawauliza.

"Yeye huyu ndiyo ananifuatafuata."

"Nani kamfuata mwenzake, mimi, wewe. Aliyekuja kwa mwenzake nani wakati umeshahama?" Akahoji Mwantumu.

"Nyinyi, sitaki kelele hapa." Polisi Jamii akaonya.

"Hivi nyinyi kinamama mbona mnatia aibu!?" Mjumbe akawauliza kwa upole na mshangao juu.

"Yaani tangu mnaishi hapa ni maneno, ugomvi kila kukicha, kila wiki nilikuwa nakuja kusuluhisha ugomvi. Haya wengine mmehama lakini bado mnakuja hapa kuleta ugomvi vipi?"

"Ndiyo ujue mjumbe kuwa huyu dada na wenzie wale pale wote walikuwa wapangaji wangu ni wagomvi."

"Mjumbe, haiwezekani huyu mama bado ananifuatafuata, mimi nimehama bado ananiambia eti nimeondoka kwake sina pesa ya kupanga kuna tajiri katuweka kwenye nyumba yake tumlindie kweli?"

"Siyo kwamba wambea wamekuja kukupa uongo?" Mjumbe akamuuliza Devota.

"Video hii hapa alipokuwa akiongea umbea wake, wenzake wamemrekodi na 'kunifowadia.'

"Kilichobaki hapa ni kwamba wote wawili, Mwantumu na Devota tunawachukua na kuwapeleka kituo cha polisi, tutawafungulia kesi ya kupigana hadharani, halafu hayo mengine tutayajadili baadaye. Na nyinyi," Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa aliwanyooshea vidole Tabia na Rozi. "Jiangalieni, ningeweza kuwaunganisha kwenye kesi hii, bahati yenu, sasa acheni chokochoko. Mmeshahama, kila mtu akae nyumbani kwake ampikie mpenzi wake au mumewe, siyo wanawake viguu na njia kufuata ugomvi." Akaonya Mwenyekiti, huku safari ya watuhumiwa kwenda kituo cha polisi ikiwa imeanza rasmi.

**"Mjumbe, haiwezekani huyu mama bado ananifuatafuata, mimi nimehama bado ananiambia eti nimeondoka kwake sina pesa ya kupanga kuna tajiri katuweka kwenye nyumba yake tumlindie kweli?"**

**MWISHO**

# MASHABIKI TABORA WAMKERA BATILDA, AWATAKA WABADILIKE

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Batilda Buruani, ameonyeshwa kukerwa na tabia ya baadhi ya mashabiki wa soka mkoani humo kushangilia timu nyingine zinapokwenda kucheza kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi dhidi ya wenyeji, Tabora United.

Batilda alisema hayo baada ya mashabiki wengi kuonekana kuzishangilia timu za Simba na Namungo zilipocheza mkoani humo hivi karibuni.

Akizungumza na wadau wa soka mkoani humo juzi, Batilda, amewataka mashabiki hao kujitathimi kama kweli wanahitaji kushuhudia michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

„Tunahitaji timu ya mkoa au tuendelee kuwa mashabiki wa klabu za Simba na Yanga?" alijohi kiongozi huyo wa mkoa.

Aliwakumbusha mashabiki wa soka wa Tabora hata kuziona klabu kubwa mkoani humo ni lazima kuhakikisha Tabora United inasalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

„Lakini ni lazima tujue ili Simba na Yanga waje Tabora ni lazima kuwe na timu itakayowaleta wachezee kwenye Uwanja wa nyumbani, timu yetu ikicheza na kufunga bao mashabiki wanaoshangilia ni wachache, lakini kwenye hizi timu kubwa uwanja mzima unashangilia, sasa unajiuliza hii timu ya Tabora United inacheza Morogoro au Dar es Salaam, ukweli aibu. Yaani kweli tukubaliane kuwa Tabora ni ya Simba na Yanga, tuendelee tu na ngoma zetu, kuhusu mpira tuendelee kushabikiwa timu kubwa tunazozijua?" alisema Batilda na kuwataka wabadilike.

Tabora United inatarajiwa kucheza dhidi ya Azam FC Jumatatu ijayo, hivyo mashabiki wametakiwa kuanza kuiunga mkono timu hiyo.

Katika msimamo wa ligi, Tabora United iko kwenye nafasi ya 14 ikiwa na pointi 16 kibindoni.

Jumanne iliyopita, Tabora United ilikipiga dhidi ya Simba na kuchapwa mabao 4-0 kwenye uwanja huo, kabla ya kucheza dhidi ya Namungo Jumapili na kuambulia sare ya bao 1-1.



Mashabiki wa Simba wakicheza nyimbo mbalimbali wakati wakiingia kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam kushuhudia timu yao ikicheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya JKT Tanzania juzi. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Matampi kinara ‚clean sheets'

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Coastal Union, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ley Matampi, anaongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mechi iliyomweka juu kipa hiyo ni ile ya kumaliza mzunguko wa kwanza waliyocheza kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam Jumatatu iliyopita dhidi ya KMC, timu hizo zikitoka suluhu.

Kwa mujibu ya takwimu zetu na za Bodi ya Ligi, kipa huyo amemaliza mzunguko wa kwanza akiwa na ‚clean sheets' saba, akifuatiwa na Yona Amosi wa Prisons ambaye anazo sita.

Golikipa wa vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Djigui Diarra, anafuatia akiwa na ‚clean sheets' tano sawa na Coastantine Malimi wa Geita Gold na John Noble wa Tabora United.

Nafasi inayofuata inakwenda kwa makipa raia wa Burundi, Jonathan Nahimana wa Namungo na Mtanzania Wilbol Maseke wa KMC.

Kwa upande wa pasi za mabao kabla ya mechi za jana, kiungo wa Azam FC, Kipre Junior, na Yao Kouassi wa Yanga, wote raia wa Ivory Coast wanaongoza wakiwa na ‚asisti' sita kila mmoja, wakifuatiwa na Impiri Mbombo wa Tabora United akiwa nazo tano.

Jumla ya wachezaji sita kila mmoja ana ‚asisti' nne, nao ni Luis Miquissone na Shomari Kapombe wa Simba, Paschal Msindo, Feisal Salum na Lusajo Mwaikenda, wote wa Azam na Awesu Awesu wa KMC.

## KMKM yatamba kutetea ubingwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kipanga hapo juzi, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM SC wamesema bado wanamatumaini kutwaa taji hilo katika msimu huu unaoendelea licha ya ushindani uliopo.

Matokeo hayo yanaifanya KMKM kufikisha pointi 38 na kuwa nyuma ya vinara JKU SC yenye alama 39, lakini bado wana mchezo mmoja pungufu.

KMKM imepata ushindi wa tatu mfululizo tangu kuanza kwa mzunguko wa lala salama wa ligi hiyo.

Mabao ya Wanamaji hao wa KMKM yalipachikwa na Ibarahim Is-haka dakika ya 14 na Ismail Bakari aliyefunga magoli dakika ya 80 na 90.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema wanaendelea vyema na mipango ya kuhakikisha lengo la kutetea taji la Ligi Kuu Zanzibar linatimia.

## Michuano kumuenzi Lina Nkya yanukia

**Na Beatrice Shayo**

FAMILIA ya Said Nkya kwa kushirikiana na Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU) wameandaa shindano linaloitwa Lina PG Tour kwa ajili ya kumwenzi nyota wa zamani wa mchezo huo, Lina Nkya ambapo washindi watajinyakulia zawadi mbalimbali, imeelezwa.

Lina Nkya alikuwa ni mchezaji wa Timu ya Taifa ya Gofu na aliwahi kupeperusha bendera ya Tanzania mwaka 2011 na kutwaa taji la Afrika Mashariki na Kati katika mashindano yaliyofanyika Dar es Salaam.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, familia hiyo na TLGU walisema lengo lao kubwa ni kutambua mchango wa Lina na kutaka kuinua vipaji kwa wanaocheza mchezo huo.

Makamu wa Rais wa TLGU, Ayne Magombe, alisema Lina alikuwa mchezaji wa gofu makini, hivyo katika kumuenzi wanataka kuendelea kuibua vipaji vipya vitakavyoiwakilisha vyema Tanzania kimataifa.

Naye kiongozi wa familia hiyo, Said Nkya (mume wa Lina) alisema mke wake alikuwa akiupenda mchezo huo kiasi cha kuibua wachezaji wengi wa kulipwa jambo ambalo wameona waliendeleze.

Katibu wa mashindano wa TLGU, Rehema Athumani, alisema mashindano hayo yatafanyika kuanzia Februari 29 hadi Machi 3, mwaka huu katika klabu ya TPC iliyopo Moshi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**OSIMHEN KUMRITHI MBAPPE**

MSHAMBULIAJI wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25, ni miongoni mwa wachezaji wanaowaniwa na Paris St-Germain kuchukua nafasi ya Kylian Mbappe (25), ambaye ameiambia klabu hiyo ya Ufaransa ataondoka mwishoni mwa msimu huu. **(Athletic)**

**ALONSO KUTUA BAYERN**

KLABU ya Bayern Munich ina uwezekano mkubwa wa kuachana na Thomas Tuchel, ifikapo msimu wa joto na wako tayari kushindana na Liverpool katika kujaribu kumteua kuinoa Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso **(Times)**

**FLICK AGOMBEWA ULAYA**

KOCHA wa zamani wa Ujerumani na Bayern Munich, Hansi Flick yuko kwenye orodha ya Barcelona ya wanaozingatiwa kuchukua nafasi ya Xavi, wakati Bayern Munich pia watamfikiria kocha huyo mwenye umri wa miaka 58 iwapo wataamua kumtimua, Thomas Tuchel. **(Bild)**

**CRYASTAL YAMNASA GLASNER**

BOSI wa zamani wa Eintracht Frankfurt, Oliver Glasner amekubali kuchukua mikoba ya Crystal Palace, ambao wanatarajiwa kuachana na Roy Hodgson. **(Times)**

**ZEBRI AITAMANI LIVERPOOL**

KLABU ya Brighton inajiandaa kwa uwezekano wa kuondoka kwa bosi, Roberto de Zerbi, mwishoni mwa msimu huu, huku Mtaliano huyo akivutiwa na Liverpool na Manchester United. **(Mail)**

**PSG YAMTAKA GAVI**

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Gavi, mwenye umri wa miaka 29 analengwa na Paris St-Germain msimu wa joto.**(Athletic)**

**MARTINELLI KUTUA BARCA**

BARCELONA inataka kuleta winga wa kushoto msimu wa joto na wanamfuatilia mchezaji wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 22, Gabriel Martinelli, nyota wa Brighton na Japan, Kaoru Mitoma (26) na Khvicha Kvaratskhelia wa Napoli (23), ambaye ni raia wa Georgia. **(Mundo Deportivo)**

**THAMANI YA SAKA HADHARANI**

ARSENAL inamthamini winga wa England, Bukayo Saka, mwenye umri wa miaka 22 kuwa na thamani ya kati ya pauni milioni 150 hadi milioni 200. (**Football Insider**)

**CHELSEA YAMWANIA KUDUS**

CHELSEA na Arsenal zinamtaka kiungo mshambuliaji wa West Ham na Timu ya Taifa ya Ghana, Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 23. **(Fichajes)**

**NORWICH YASAKA KOCHA**

KLABU ya Norwich City imeonyesha nia ya kumbadilisha Kocha, David Wagner na kumchukua Kocha Msaidizi wa Arsenal, Carlos Cuesta, ifikapo msimu wa joto **(Guardian)**

**UNITED KUILIPA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle United imeonyesha imani inaweza kudai ada ya fidia ya zaidi ya pauni milioni 10 ikiwa Mkurugenzi wa Michezo, Dan Ashworth, ataondoka katika klabu hiyo na kujiunga na Manchester United.**(Standard)**

## DON… O ZA SOKA M… YA ULAYA




# MBAPPE RASMI ANAONDOKA PSG

●●●Mshambuliaji huyo wa Ufaransa aweka wazi nia yake, Madrid...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe, ameiambia Paris St-Germain ana nia ya kuondoka katika klabu hiyo ifikapo mwishoni mwa msimu huu.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 na mabingwa hao wa Ligue 1 unakaribia kumalizika na amekuwa akihusishwa kujiunga na Real Madrid.

Mustakabali wa Mbappe ulikumbwa na mzozo mkubwa na PSG msimu uliopita wa joto.

Wakati fulani, Mbappe alifukuzwa kwenye kikosi cha kwanza na kuachwa nje ya ziara ya klabu hiyo ilipokwenda kufanya maandalizi ya msimu mpya barani Asia.

Lakini makubaliano yalifikiwa ambayo yalihakikisha PSG haitapoteza wakati Mbappe atakapoondoka na masharti ya kuondoka kwake ambayo sasa inaonekana haiwezi kuepukika.

Mshambuliaji huyo ana kipengele cha kuongeza mwaka mmoja, hivyo inatarajiwa kuondoka kwake kutahusisha ama mauzo na ada ya uhamisho au fidia za kifedha kwa upande wa mchezaji.

Ingawa PSG wangetaka Mbappe abaki klabuni hapo, kuondoka kwake kunaonekana kuja huku wakilenga kujenga kikosi cha vijana.

Inakadiriwa Mbappe, ambaye alishinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018, anapokea takribani euro milioni 200 kwa mwaka.

# TUCHEL KUTUPIWA VIRAGO NA BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, inaonekana huenda kuna uwezekano mkubwa wa kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.


Matokeo yasiyoridhisha katika wiki za hivi karibuni yamefikia kilele katika siku chache zilizopita baada ya kuchapwa mabao 3-0 na wapinzani wao wa Bundesliga, Bayer Leverkusen na kupoteza mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora na Lazio.

90min imeripoti kuna dalili zinazoongezeka ambapo Tuchel anaweza kuondoka msimu wa joto au mapema zaidi.

Kuna maoni Bayern Munich haijawa na wakati mzuri tangu Tuchel aajiriwe kuchukua nafasi ya Julian Nagelsmann, ambaye alifutwa kazi miezi 11 iliyopita licha ya asilimia 71.4 ya ushindi.

Wachezaji kama Jamal Musiala hawajaanza chini yake, huku akionekana kukosa majibu ya kutatua masuala hayo.

Bayern Munich walitaka kuepuka kuachana na kocha katikati ya msimu, huku klabu hiyo ikikaribia kupokonywa taji la Bundesliga.



Bado kuondoka kwa Tuchel kunaweza kuharakishwa ikiwa hakutakuwa na uboreshaji wa haraka wa kikosi hicho.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 50, ambaye ana mkataba na Bayern Munich hadi mwaka 2025, hapo awali aliiongoza Chelsea kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021 na alikuwa kocha aliyeiongoza Paris Saint-Germain kwenye fainali yao pekee ya michuano hiyo ya Ulaya.

Alikuwa mtu aliyechaguliwa kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp huko Dortmund mnamo 2015, pia hapo awali alitengeneza jina lake katika klabu nyingine kama Mainz.

Kocha wa mwisho wa Bayern Munich kushindwa kushinda taji la Bundesliga alikuwa Jupp Heynckes mnamo msimu wa 2011/12 - pia msimu wa mwisho wa klabu bila taji - ingawa bado aliwaongoza hadi fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya 2012.

## Ivory Coast 'waoga' zawadi

**ABIDJAN, Ivory Coast**

WACHEZAJI wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast na Kocha Mkuu wa muda, Emerse Fae, wamepewa fedha na nyumba za kifahari baada ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kwa kuifunga Nigeria mabao 2-1 kwenye ardhi yao ya nyumbani.

Kila mchezaji kwenye kikosi cha timu hiyo amepewa faranga za Ivory Coast milioni 50 sawa na Dola za Marekani 82,152 na nyumba za kifahari zenye thamani inayolingana na kiasi hicho cha fedha.

Fae amepokea faranga milioni 100 kwa kuiongoza timu hiyo kushinda ubingwa akichukua nafasi ya Jean-Louis Gasset katikati ya mashindano baada ya timu hiyo kufungwa mabao 4-0 na Guinea ya Ikweta.

"Mmeleta furaha kwa watu wa Ivory Coast, hongereni sana," alisema Rais wa nchi hiyo, Alassane Ouattara.

Wachezaji pia walitunukiwa tuzo ya heshima kubwa kuliko zote kwenye taifa la Ivory Coast kwa mafanikio hayo.

Hilo ni taji la tatu kwa Ivory Coast kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).



## Suarez kustaafia Inter Miami

**MIAMI, Marekani**

INTER Miami itakuwa klabu ya mwisho kwa Luis Suárez kuichezea, mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Uruguay, amesema.

Suárez mwenye umri wa miaka 37, alijiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS), mwaka jana kwa msimu wa 2024 baada ya kuitumikia Gremio ya Brazil.

Aliungana na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi, Sergio Busquets na Jordi Alba, ambaye alishinda nao mataji manne ya LaLiga ndani ya miaka mitano, Hispania.

"Inter Miami itakuwa klabu yangu ya mwisho, familia yangu tayari inajua hilo. Sina tarehe bado, lakini ni hatua ya mwisho," alisema Suárez katika mahojiano na kituo cha redio cha Uruguay, Del Sol.

"Niko tayari kwa changamoto hii ya mwisho, lakini kuna uchovu usioepukika na, mwishowe, nataka kuwa na maisha bora katika siku zijazo," aliongeza.

Suárez, ambaye pia alizichezea Ajax Amsterdam, Liverpool na Atlético Madrid, amecheza mechi 138 akiwa na Uruguay tangu mwaka 2007.



# SHIME AANIKA MAJEMBE YAKE ALL AFRICAN GAMES

**Na Saada Akida**

WAKATI akiweka hadharani wachezaji wanaounda kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), kwa ajili ya kushiriki Michezo ya Afrika (All African Games), Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema anaamini watafanya vizuri katika michuano hiyo wakiwa imara.

Tanzanite imepata nafasi ya kushiriki Michezo ya Afrika itakayofanyika Accra, Ghana baadaye mwezi ujao.

Shime pia ndio Kocha Mkuu wa Twiga Stars ambayo inakibarua cha kuwakaribisha Afrika Kusini maarufu Banyana Banyana itakayochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kocha huyo alisema nguvu na akili zao kwa sasa wanazielekeza katika mchezo uliopo mbele yao dhidi ya Afrika Kusini wa kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki na wanajiandaa kuhakikisha wanafikia malengo.

Alisema tayari ameshaanza kuwafuatilia wapinzani wao (Afrika Kusini) na wanajipanga kuanza vyema hapa nyumbani ili kujiweka kwenye nafasi nzuri watakaporudiana ugenini.

Alisema licha ya kutafuta ushindi lakini anatumia mechi hiyo kama maandalizi kuelekea michezo yao ya All Afrika Games baada ya baadhi ya nyota wake wa Tanzanite kuwepo sehemu ya kikosi cha Twiga Stars.

Aliongeza baadhi ya wachezaji waliopo Tanzanite pia wanaichezea Twiga Stars na amefanya hivyo ili kuwaongezea uzoefu zaidi nyota hao.

Kikosi cha Tanzanite kinaundwa na Husna Mtunda (Yanga Princess), Winifrida Gerald, Christer Bahera, Jamila Rajabu, Joyce Lema (JKT Queens), Violeth Nicholaus, Aisha Mnunka (Simba Princess), Hasnat Ubamba (Fountain Gate Princess), Zulfa Makau, Lydia Maximilian, Jackline Shija na Alia Fikiri (JKT Queens), Mariam Shaban, Esther Maseke, Jamila Selestine (Bunda Queens).

Wengine ni Sarah Joel (Fountain Gate Princess), Koku Kipanga, Zainabu Mohammed (Simba Queens), Sabina Alex (Geita Gold Queens ), Neema Paul na Asha Omari (Yanga Princess).

Katika Michezo ya Afrika, Tanzanite iko Kundi A pamoja na wenyeji Ghana , Uganda na Ethiopia.

# JKT TZ yalia na washambuliaji

**Na Oliver Albert**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Malale Hamsini, amewataka washambuliaji wake kubadilika na kuongeza kasi ya kufunga mabao kwa sababu wako katika nafasi mbaya kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Maafande hao wakiikaribisha kwa mara ya kwanza Simba kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni walikubali kichapo cha bao 1-0.

Malale alisema kama washambuliaji wake wangetumia vyema nafasi walizotengeneza katika mechi dhidi ya Simba iliyochezwa juzi, wangeibuka na ushindi.

Kocha huyo alisema katika mchezo huo walitengeneza nafasi nne za wazi lakini washambuliaji wake walimwangusha.

„Ukiangalia sisi ndio tulitengeneza nafasi nyingi kuliko Simba, tena nne za wazi kabisa, washambuliaji wangu wakitizamana na kipa lakini wakazitupa, wenzetu walipata mbili tu na moja wakatumia wakashinda mechi.

Yaani washambuliaji wangu walikuwa si wa kukosa mabao, tena katika mechi ngumu kama hii na ukizingatia sisi tulitengeneza nafasi nyingi, „ alisema Malale na kuongeza;

„Jambo ninalotaka kuwaambia washambuliaji wangu kuwa ishu ya kufunga ni ya mchezaji mwenyewe, kocha kazi yake ni kuhakikisha timu inafika eneo la kufunga hivyo sasa wanatakiwa kujiongeza, ligi ni ngumu na hatuko sehemu salama hivyo lazima tuongeze juhudi ya kupambana ili tutoke nafasi tuliyopo,“ alisema Malale.

Katika msimamo wa ligi, JKT Tanzania iko kwenye nafasi ya 13 ikiwa na pointi 16 baada ya kucheza michezo 15, imeshinda mechi nne, imetoka sare michezo minne na kupoteza michezo saba.




Wachezaji chipukizi wanaolelewa katika kituo kinachosimamiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kilichoko Mnyanjani jijini, Tanga wakifanya mazoezi ili kuendeleza vipaji vyao. **PICHA: TFF**

## Yanga, KMC FC vitani Morogoro

INATOKA UK. 24

(Twiga Stars na Taifa Stars), ili kuunganisha nguvu za pamoja zitakazoliheshimisha taifa.

Akizungumza jana, wakati akitoa hotuba yake ya kuahirisha mkutano wa 14 wa Bunge la 12, Majaliwa, alisema zoezi la harambee bado linaendelea, ni vyema Watanzania wote wakachangia kupitia namba zitakazotangazwa.

"Nitumie nafasi hii, kuwasihi sana Watanzania wote kuendelea kuchangia timu zetu za Taifa. Zoezi la Harambee bado linaendelea Watanzania wote tuchangie kupitia namba zitakazotangazwa.

Wizara ya michezo bado inaendelea kuratibu zoezi la uchangiaji. Kama wahenga walivyosema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Tuunganishe nguvu za pamoja ili tuweze kufanikiwa na kuliheshimisha Taifa letu kupitia sekta ya michezo."

Mbali na kujiandaa na michuano mbalimbali ya kimataifa, Tanzania, Kenya na Uganda zinajiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027), baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuwatangaza na nchi hizo za ukanda wa CECAFA (Shirikisho la Vyama vya Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na Kati), umeandika historia mpya katika soka baada kupewa tiketi ya kuwa wenyeji fainali hizo.

**Imeandaliwa na Adam Fungamwango na Saada Akida, DAR na Godfrey Mushi, DODOMA**

## BENCHIKHA ANG'AKA, CHAMA AOTA KOMBE

INATOKA UK. 24

mashambulizi na kurudi nyuma kwa haraka kukaba kama ilivyokuwa kwa viungo, Sadio Kanoute na Babacar Sarr, ambao kila mara aliwakumbusha kurudi nyuma kusaidia ulinzi.

Naye Kocha Msaidizi wa Simba, Daniel Cadena, amekiri wamekuwa na siku chache ngumu za mechi mfululizo lakini hata hivyo amewasifu wachezaji wake kwa kuendelea kupambana na kupata ushindi.

„Ni ngumu kucheza mfululizo mechi nyingi katika muda mfupi lakini wachezaji wameendelea kupambana kuhakikisha tunapata matokeo, wanastahili pongezi kwani licha ya kwamba mechi ni ngumu lakini jambo muhimu ni kupata pointi tatu, „ alisema Cadena.

Katika hatua nyingine, Chama amesema licha ya kwamba wamemaliza mzunguko wa kwanza wakiwa nafasi ya pili katika msimamo wa ligi na kuzidiwa pointi nne na wapinzani wao, Yanga lakini hilo haliwafanyi kukata tamaa ya kufikia malengo ya kutwaa ubingwa.

Mchezaji huyo raia wa Zambia alisema kama timu wanaendelea kujitafuta kwa kuhakikisha kila mara wanapunguza makosa katika michezo yao.

„Tulikuwa na makosa kidogo katika baadhi ya mechi zetu lakini kila wakati tumekuwa tukirekebisha ili kuwa bora zaidi. „Tumezidiwa pointi nne na walio juu yetu hilo halitukatishi tamaa bali tunaendelea kupambana kuhakikisha malengo yetu ya kutwaa ubingwa msimu huu yanatimia,“ alisema Chama.

Michezo
Jumamosi Februari 17, 2024
Nipashe

## Suarez kustaafia Inter Miami

UKURASA 22



# YANGA, KMC FC VITANI MORO

### Gamondi atabiri mechi ngumu, Majaliwa awaangukia wadau...

**Na Waandishi Wetu**

MABINGWA watetezi, Yanga watakuwa ugenini kuwakabili KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro ambapo Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, amesema michezo ya hivi karibuni imekuwa migumu kwa vinara hao.

KMC, yenye maskani yake Kinondoni, Dar es Salaam imeamua kupeleka mechi yake ya nyumbani mkoani humo kutokana na kuruhusiwa na kanuni.

Gamondi alisema anafahamu mechi hiyo haitakuwa rahisi hata kidogo na watakachokwenda kukifanya ni kusaka pointi tatu na si kwenda kuburudisha licha ya yeye kupenda soka la aina hiyo.

„Mara zote huwa napenda kucheza mchezo wa kuburudisha lakini huu hautakuwa mchezo rahisi, ila tupo hapa kwa ajili ya kufanya vizuri ili kutimiza malengo,“ alisema Gamondi.

Hata hivyo alikiri kila mechi zinavyozidi kwenda mbele zinazidi kuwa ngumu na akasema inawezekana ligi ya msimu huu inaushindani kuliko msimu uliopita.

„Sikuwepo msimu uliopita, lakini inawezekana ligi hii ikawa ngumu zaidi, siwezi kusema sana kwa sababu mimi ni sehemu ya benchi la ufundi, lakini nafurahi sana kuona ugumu kwenye baadhi ya mechi kwa sababu inafanya ligi kuwa na ubora,“ Gamondi alisema.

Kocha huyo alisema kutokana na hilo, kwa sasa wanachoangalia zaidi ni pointi tatu kuliko idadi ya mabao kwani kila timu kwa sasa imesajili na kujidhatiti na haiwezekani kupata ushindi kirahisi.

Beki na kulia anayekuja kwa kasi, Nickson Kibabage, alisema timu yao imefanya maandalizi mazuri na wamejiandaa na mchezo huo dhidi ya ‚timu nzuri' ya KMC.

„Raundi ya pili huwa ni ngumu lakini kwa ukubwa wa klabu ya Yanga tunahitaji kushinda kila mechi, sisi wachezaji kila sehemu tunayokwenda huwa tunatambua umuhimu wa mechi na tunaamini katika kuwapa furaha mashabiki, „ alisema Kibabage.

Kocha wa KMC, Abdihamid Moalin, alisema wanakwenda kucheza na timu nzuri nchini na kutokana na hilo amewaonya wachezaji wake kutofanya makosa ya kujirudia mara kwa mara na hasa kwa upande wa mabeki.

Nahodha wa KMC, Awesu Awesu, kwa upande wake amesema wana morali na wako tayari kupambana na Yanga.

„Tulicheza na Yanga mwanzo, tulifungwa mabao matano, lakini kumbuka kipindi kile ligi ndiyo kwanza ilikuwa inaanza, hatukuwa sawa, haiwezekani tukaenda na akili zile zile,“ alisema Awesu.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewasihi Watanzania kujitokeza kuchangia timu za taifa za



Gamondi

INAENDELEA UK. 23



Lakred

# Benchikha ang'aka, Chama aota kombe

**Na Oliver Albert**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, aligeuka mbogo kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa juzi huku kiungo wake, Clatous Chama, akisema bado wana nafasi ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Benchikha alionekana akiwafokea wachezaji wake pindi waliposhindwa kufanya kile alichotaka uwanjani katika mechi hiyo walioondoka na ushindi wa bao 1-0.

Nipashe lilishuhudia kocha huyo kila wakati akifoka huku akirusha mikono na wakati mwingine kuwaonyesha wachezaji wake kwa mifano jinsi wanavyotakiwa kucheza uwanjani.

Mechi tano ndani ya siku 12 inadaiwa ndio chanzo cha wachezaji wa Simba kuchoka uwanjani na ni kama ilivyo kwa wapinzani wao wakubwa Yanga ambao wamecheza mechi nne ndani ya siku 10.

Juzi katika mchezo dhidi ya JKT wachezaji wengi wa Simba walioneka wazito na kutokaba kwa ufasaha hivyo kuruhusu mashambulizi mengi golinj kwao jambo lililokuwa likimkasirisha Benchika kila wakati na kufoka.

Kocha huyo raia wa Algeria kila mara alikuwa akiwaita kwa majina wachezaji wake na kuwataka kukaba sana pindi timu yao ilipokuwa haina mpira kwa kila mchezaji kuhakikisha mpinzani hapati nafasi ya kushambulia.

Pia alikuwa akiwataka wakiwa na mpira kupandisha mashambulizi mbele kwa haraka na kuacha kupiga pasi za nyuma na pia kuwa na uwezo wa kutuliza mpira na kuacha papara.

Beki wa pembeni Shomari Kapombe, ni mmoja ya wachezaji waliionja joto la kufokewa kila mara na Benchika akitakiwa kupanda mbele kupeleka

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >